JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA KIDATO CHA PILI (FTNA) 2024

## ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA KIDATO CHA PILI (FTNA) 2024

# 015 ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

*Kimechapishwa na*:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2025**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO


DIBAJI ..... iv

1.0 UTANGULIZI ..... 1

2.0 UCHAMBUZI WA KILA SWALI ..... 2

2.1 Sehemu A: Kuchagua Jibu Sahihi na Kuoanisha ..... 2
2.1.1 Swali la 1: Kuchagua Jibu Sahihi ..... 3
2.1.2 Swali la 2: Nguzo za Uislamu ..... 13
2.2 Sehemu B: Majibu Mafupi ..... 17
2.2.1 Swali la 3: Kumjua Mwenyezi Mungu ..... 17
2.2.2 Swali la 4: Mtazamo wa Uislamu Juu ya Ibada ..... 21
2.2.3 Swali la 5: Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti wa Kiislamu ..... 26
2.2.4 Swali la 6: Qur'an ..... 30
2.2.5 Swali la 7: Sunnah na Hadithi ..... 33
2.2.6 Swali la 8: Historia katika Uislamu. ..... 36
2.2.7 Swali la 9: Bara Arab Zama za Jahiliyyah Karne ya 6 A.D. ..... 41
2.3 Sehemu C: Insha ..... 45
2.3.1 Swali la 10: Nguzo za Uislamu ..... 45

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KWA KILA MADA ..... 50

4.0 HITIMISHO ..... 51

5.0 MAPENDEKEZO ..... 51

Kiambatisho cha Pekee ..... 52

Uchambuzi wa Ufaulu wa Wanafunzi katika Mada ..... 52

**DIBAJI**

Uchambuzi huu unaonesha majibu ya wanafunzi katika Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili (FTNA) 2024 katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu. Makusudio ya uchambuzi huu ni kutoa mrejesho kwa wadau wa elimu kuhusu viwango vya ufaulu wa wanafunzi katika upimaji wa somo hili, na kubainisha sababu mbalimbali zilizochangia katika ufaulu huo.

Taarifa hii imebainisha sababu zilizochangia matokeo ya wanafunzi hao kupata alama za juu, wastani na za chini katika kila swali. Aidha, sampuli za majibu ya wanafunzi waliofanya vizuri na wale waliofanya vibaya zimeoneshwa. Sababu zilizowawezesha baadhi ya wanafunzi kujibu maswali kwa usahihi ni pamoja na; kuwa na ufahamu wa kutosha katika mada zilizopimwa, kuelewa matakwa ya maswali yaliyoulizwa na uwezo wa kuwasilisha hoja kwa usahihi. Pia, uchambuzi huu umebaini kuwa wanafunzi walioshindwa kujibu maswali kwa usahihi, baadhi yao hawakuwa na ujuzi wa kutosha katika mada mbalimbali za Elimu ya Dini ya Kiislamu, wengine kushindwa kubaini matakwa ya maswali katika mada husika na wengine kushindwa kuwasilisha hoja kwa usahihi.

Baraza la Mitihani lina imani kuwa, mrejesho huu utawawezesha walimu, wanafunzi, wazazi, watunga sera na wadau wote wa elimu kuchukua hatua madhubuti za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, hatimaye kuondoa changamoto zilizobainishwa katika taarifa hii. Endapo mapendekezo yaliyotolewa mwishoni mwa taarifa hii yatazingatiwa, ni imani ya Baraza kuwa kiwango cha ufaulu katika somo hili kitaongezeka.

Baraza la Mitihani linatoa shukrani za dhati kwa wote waliohusika katika uandishi wa taarifa hii.



Dkt. Said Ally Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inahusu uchambuzi wa majibu ya wanafunzi waliofanya Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili (FTNA) Novemba 2024 katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu. Upimaji huu uliandaliwa kwa kuzingatia muhtasari wa somo wa mwaka 2012 wa Kidato cha I na II.

Maswali yaliandaliwa kutoka katika mada kumi ambazo ni: *Mtazamo wa Uislamu Juu ya Elimu, Mtazamo wa Uislamu Juu ya Dini, Mtazamo wa Uislamu Juu ya Ibada, Nguzo za Uislamu, Qur'an, Sunnah na Hadithi, Bara Arab Zama za Jahiliyyah, Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti wa Kiislamu, Historia katika Uislamu* na *Kumjua Mwenyezi Mungu*. Maswali hayo yaligawanywa katika sehemu tatu; A, B na C zenye jumla ya alama 100. Sehemu A ilikuwa na maswali mawili (1 na 2), sehemu B ilikuwa na maswali saba (3, 4 ,5, 6, 7, 8 na 9) na sehemu C ilikuwa na swali moja (10). Mwanafunzi alitakiwa kujibu maswali yote kumi (10).

Wanafunzi waliosajiliwa kufanya upimaji wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu mwaka 2024 walikuwa 113,806 kati yao wanafunzi 104,014 sawa na asilimia 91.39 walifanya upimaji. Idadi hiyo, inaonesha kuwepo kwa ongezeko la wanafunzi 16,512, ikilinganishwa na wanafunzi 87,502 waliofanya upimaji wa somo hili mwaka 2023. Kati ya wanafunzi 104,014 waliofanya upimaji mwaka 2024, wanafunzi 74,176 sawa na asilimia 71.41 walifaulu katika madaraja mbalimbali. Jedwali lifuatalo linaonesha madaraja ya wanafunzi hao ikilinganishwa na mwaka 2023.

**Jedwali Na. 1: Ulinganifu wa Ufaulu Kati ya Mwaka 2024 na 2023**

| **Mwaka** | **Asilimia ya Ufaulu** | **Madaraja** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | A | B | C | D | F |
| 2024 | 71.41 | 789 | 3,014 | 28,512 | 41,861 | 29,695 |
| 2023 | 68.32 | 200 | 1,586 | 21,586 | 36,249 | 27,651 |

Takwimu zilizopo katika Jedwali Na. 1 zinaonesha kuwa kiwango cha ufaulu kwa mwaka 2024 kimeongezeka kwa asilimia 3.09

ikilinganishwa na mwaka 2023. Vilevile, idadi ya wanafunzi waliopata daraja A mwaka 2024 imeongezeka kwa asilimia 59.56 ikilinganishwa na mwaka 2023, huku idadi ya wanafunzi waliopata daraja B ikiongezeka kwa asilimia 31.04 ikilinganishwa na mwaka 2023.

Taarifa hii imechambua majibu ya wanafunzi katika kila swali kwa kuzingatia matakwa ya swali husika, majibu sahihi ya swali hilo na yale waliyotoa wanafunzi katika swali hilo. Aidha, sampuli za majibu ya wanafunzi zimeambatanishwa ili kuonesha namna wanafunzi walivyojibu maswali. Taarifa hii imebainisha changamoto zilizowakabili wanafunzi katika kujibu kila swali na kiwango cha ufaulu katika mada mbalimbali zilizopimwa. Aidha, madaraja ya ufaulu katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu yalikuwa kama ifuatavyo:

**Jedwali Na. 2: Madaraja ya Ufaulu Elimu ya Dini ya Kiislamu**

| Alama | Daraja | Maoni |
|---|---|---|
| 75 – 100 | A | Bora |
| 65 – 74 | B | Vizuri Sana |
| 45 – 64 | C | Vizuri |
| 30 – 44 | D | Inaridhisha |
| 0 – 29 | F | Dhaifu |

Jedwali Na. 2 linaonesha kuwa daraja la juu zaidi la ufaulu katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu ni A na daraja la chini zaidi ni F. Pamoja na kuwa na madaraja matano ya ufaulu kama yalivyooneshwa, taarifa hii itatumia madaraja matatu katika kuwasilisha ngazi za ufaulu ambayo ni: **vizuri, wastani** na **dhaifu**. Ufaulu ulikuwa dhaifu ikiwa asilimia ya wanafunzi waliofanya vizuri katika swali ni 0 hadi 29. Ufaulu ulikuwa wa wastani ikiwa waliofaulu swali ni kati ya asilimia 30 hadi 64 na ufaulu ni mzuri ikiwa ni asilimia 65 hadi 100.

## 2.0 UCHAMBUZI WA KILA SWALI

### 2.1 Sehemu A: Kuchagua Jibu Sahihi na Kuoanisha


Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili ambayo mwanafunzi alitakiwa kujibu maswali yote. Swali la kwanza lilikuwa la kuchagua jibu sahihi katika vipengele kumi (i) – (x), ambapo kila kipengele kilikuwa na

alama moja (01), hivyo kuwa na jumla ya alama kumi (10). Swali la pili lilikuwa la kuoanisha, ambalo lilikuwa na vipengele vitano (i) – (v), ambalo lilikuwa na alama tano (05) sawa na alama moja (01) kwa kila kipengele. Hivyo, sehemu A ilikuwa na jumla ya alama 15.

### 2.1.1 Swali la 1: Kuchagua Jibu Sahihi

Katika swali hili wanafunzi walitakiwa kuchagua herufi ya jibu sahihi kutoka katika machaguo manne waliyopewa (A, B, C na D), kisha kuandika herufi ya jibu hilo katika kisanduku. Swali hili lilipima ngazi mbalimbali za umahiri katika mada za *Mtazamo wa Uislamu Juu ya Elimu, Mtazamo wa Uislamu Juu ya Dini, Nguzo za Uislamu, Qur'an, Sunnah na Hadithi* na *Bara Arab Zama za Jahiliyyah.*

Wanafunzi wote 104,014 (100 %) walijibu swali hili. Kati ya wanafunzi hao, 72,491 (69.69%) walipata alama 3 hadi 6, ambao ni ufaulu wa wastani. Wanafunzi 26,321 (25.31%) walipata alama 0 hadi 2, ambao ni ufaulu dhaifu. Na wanafunzi 5,202 (5.00%) walipata alama 7 hadi 10, ambao ni ufaulu mzuri. Muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao ni kama inavyoonekana katika Chati Na. 1.




**Chati Na. 1**: *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 1*

Chati Na. 1 inaonesha kuwa ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani asilimia 74.69 kati ya wanafunzi wote walijibu kwa usahihi, hatimaye kupata alama 3 hadi 10. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada mbalimbali zilizounda vipengele kumi vya swali la kwanza. Aidha, uchambuzi wa majibu ya wanafunzi hao katika kila kipengele umebainishwa kama ifuatavyo:

Kipengele (i) mwanafunzi alitakiwa kubaini mgawanyo sahihi wa elimu kwa mujibu wa mafundisho ya Uislamu. Kipengele hiki kilipima uwezo wa mwanafunzi kuelewa dhana ya elimu katika Uislamu, ambapo wanafunzi walioelewa vema dhana hiyo, waliweza kubaini jibu sahihi D; *Elimu ya mwongozo na elimu ya mazingira,* kwakuwa mgawanyo huo ulibainishwa wazi katika Qur’an (2:31 na 2:38). Katika aya hizo, Mwenyezi Mungu Mtukufu anabainisha kuwa alimpa Nabii Adamu (A.S) Elimu ya fani mbalimbali za kimazingira na asili ya vitu ili aweze kumudu vema mazingira yake. Hata hivyo, kwakuwa elimu ya mazingira pekee haitoshi kumuwezesha kufikia lengo la kuumbwa kwake, Mwenyezi Mungu akampa pia elimu ya mwongozo ili kujua matumizi sahihi ya mazingira yake katika maisha ya hapa duniani, kwa ajili ya mustakbali mzuri baada ya kuondoka kwake hapa duniani.

Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki, baadhi yao walichagua kipotoshi A; *Elimu dunia na elimu akhera,* kwa sababu ya kutawaliwa na dhana potofu juu ya mgawanyo wa elimu, kwa kuinasibu elimu ya mwongozo na maisha ya akhera na elimu ya mazingira na maisha ya duniani, ilihali elimu zote zimekusudiwa kutumika hapa duniani. Wengine walichagua herufi B; *Elimu ya mwongozo na elimu ya Qur’an* na C; *Elimu ya mazingira na elimu ya shule*. Kadhalika, wanafunzi walidhihirisha kuwa walikosa maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya elimu katika Uislamu, kiasi cha kushindwa kutambua kuwa vipotoshi vyote viwili, ambavyo vilikuwa vinataja dhana moja pamoja na njia inayoweza kutumika kupata elimu.

Katika kipengele cha (ii) mwanafunzi alitakiwa kubainisha hoja inayoeleza kazi kuu ya Dini katika maisha kwa mujibu wa Uislamu. Kipengele hiki kilipima uwezo wa mwanafunzi kuchambua dhana ya Dini kwa mujibu wa Uislamu, ambapo wanafunzi hodari katika mada ya Mtazamo wa Uislamu juu Juu ya Dini, waliweza kubaini jibu sahihi B;

*Kuwanusuru watu katika namna zote za uonevu.* Wanafunzi hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya Dini kwa mujibu wa Uislamu, ambapo moja kati ya tafsiri zake ni kujisalimisha kikamilifu katika matakwa ya Mwenyezi Mungu. Tafsiri hiyo inabeba ndani yake kazi ya msingi ya dini, ambayo ni kuwatoa watu chini ya utii mwingine wote na kuwaweka huru dhidi ya aina zote za uonevu.

Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hiki, walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu kazi ya msingi ya Dini kwa mujibu wa Uislamu, hivyo walichagua vipotoshi A; *Kuweka njia ya mahusiano baina ya watu,* C*; Kufafanua asili ya wanadamu na malengo yao* na D; *Kukamilisha hitajio la mtu kiroho na kiitikadi*. Machaguo hayo, hayakuwa sahihi kwa sababu yalitaja miongoni mwa kazi ndogo za dini, badala ya kazi kuu kama ilivyotakiwa katika hoja ya kipengele hiki.

Kipengele cha (iii) mwanafunzi alitakiwa kuchagua aina ya Hijjah iliyo nafuu kwa mtu anayetoka mbali ya mji wa Makkah. Swali hili lilimpima mwanafunzi uwezo wa kuelewa aina za Hijjah na namna zinavyo tekelezwa. Wanafunzi mahiri katika mada hiyo, waliweza kubaini jibu sahihi na kuchagua herufi A; *Tamattu.* Aina hii ya Hijjah inakuwa nafuu kwa sababu inamruhusu mtu anayehiji kutoka katika masharti ya Hijjah (*Ihramu*) na kuwa huru, kisha kurudi tena kuanzia tarehe nane (08) Dhulhijah na kuendelea na matendo ya Hijjah hadi mwisho.

Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki, baadhi yao walichagua vipotoshi B; *Qiraan* na D; *Ifraad.* Machaguo hayo, yaliashiria kukosa elimu ya kutosha kuhusu aina za Hijjah, kwani hayakuwa sahihi kuwa katika aina hizo, Hajji analazimika kubaki katika *Ihramu* muda wote hadi atakapokamilisha matendo ya Hijjah. Hivyo, aina hizi hazina nafuu kwa mwenye kuhiji anayetoka mbali. Waliochagua kipotoshi C; *Umrah,* walionesha kushindwa kufasiri muktadha wa swali, pia walikosa maarifa ya jumla ya ki-fiqh juu ya vipaumbele vya ibada, kwani Umrah ni ibada ya Sunnah, ambayo inaweza kutekelezwa wakati wowote, wakati Hajjih ni Faradh, ambayo ni lazima mara moja katika maisha, hivyo yampasa mtu kuanza nayo kabla ya Umrah.

Katika kipengele cha (iv) mwanafunzi alitakiwa kubaini aina ya kafara, inayomlazimu Muislamu kutekeleza baada ya kuvunja kiapo halali. Kipengele hiki, kilipima uwezo wa mwanafunzi kukumbuka aina mbalimbali za Funga, ambazo sharia imeziweka kama njia ya kutakasa makosa. Aidha, wanafunzi mahiri katika Funga za kafara waliweza kukumbuka kwa usahihi hukumu hiyo na kuandika herufi C; *Kufunga siku tatu mfululizo*, kwani maelekezo ya sharia juu ya kafara kwa mtu aliyevunja kiapo halali ni kufunga siku tatu mfululizo.

Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki, walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu funga za kafara. Baadhi ya wanafunzi hao walichagua kipotoshi A; *Kufunga miezi mitatu bila kuacha,* jambo ambalo sio sahihi kwakuwa haliendani na maelekezo yoyote ya kisheria. Wengine walichagua B; Kufunga *siku saba mfululizo,* kafara ambayo anaifanya mtu aliyevunja sharti la *Ihram*, ambapo Hajji atalazimika kufunga siku tatu akiwa Hija na kumalizia siku saba atakaporejea. Aidha, waliochagua kipotoshi D; *Kufunga miezi miwili.* Walishindwa kufahamu kuwa hiyo ni kafara inayowahusu watu walioshiriki tendo la ndoa katika mchana wa Ramadhani.

Kipengele cha (v) mwanafunzi alitakiwa kukokotoa kiwango cha nafaka kinachopaswa kutolewa na mtu mwenye mke mmoja mjamzito na watoto wanne, ambao mmoja wapo ni wakulea na sio Muislamu. Kipengele hiki kilipima uwezo wa mwanafunzi kutumia maarifa yake kuhusu Zakat Fitr katika miktadha mbalimbali. Aidha, wanafunzi mahiri katika Fiqh ya Funga ya Ramadhan, waliweza kukokotoa kiasi stahiki kulingana na ukubwa wa familia hiyo na kupata jibu sahihi B; *Kg 12.5.* Wanafunzi hao waliweza kubaini waliostahiki kutolewa Zakat Fitr, ambao ni yeye mwenye nyumba, mkewe na watoto watatu, kwani mtoto ambae hajazaliwa na yule wakulea ambae si Muislamu hawatolewi Zakat Fitr. Kadhalika, walifahamu kiwango cha nafaka kinachotolewa kwa kila anayestahiki, ambacho ni kilo 2.5. Hivyo, 2.5 x 5 = Kilo 12.5.

Kwa upande mwingine, wanafunzi walioshindwa kujibu kipengele hiki kwa usahihi, baadhi yao walichagua kipotoshi A; *Kg10*, ambacho ni kwa hesabu ya watu wanne badala ya watano, wakihisi kuwa mjamzito hatolewi Zakat Fitr. Wengine walichagua C; *Kg15*, kwa kumjumuisha mtoto wa kulea katika wanaostahiki, jambo ambalo sio sahihi.

Kadhalika, wapo waliochagua kipotoshi D; *Kg17.5*, wakipiga hesabu kwa watoto wote pamoja na yule ambae bado hajazaliwa. Aidha, baadi ya wanafunzi walichagua vipotoshi hivi kwa msingi wa kubahatisha kwa kuwa walikosa maarifa ya kutosha kuhusu Fiqh ya Zakat Fitr.

Katika kipengele cha (vi) mwanafunzi alitakiwa kubaini idadi ya mafungu, ambayo Mtume (S.A.W) aliwaamrisha maswahaba wake kukusanya na kuiandika Qur'an hapo mwanzo. Kipengele hiki kilipima uwezo wa wanafunzi kukumbuka kwa usahihi vipengele muhimu katika historia ya kukusanywa na kuhifadhiwa Qur'an kipindi cha Mtume Muhammad (S.A.W). Wanafunzi mahiri katika historia ya Qur'an, waliweza kukumbuka vema mchakato wa kukusanywa na kuandikwa Qur'an, hivyo walichagua herufi A; *Saba,* wanafunzi hao walikumbuka kwa usahihi agizo hilo, ambalo limenukuliwa na waandishi mbalimbali wa Hadithi (Rawi), kutoka katika Sanad ambazo hazina mashaka.

Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki, walionesha kukosa maarifa kuhusu historia ya kukusanywa na kuhifadhiwa Qur'an. Baadhi ya wanafunzi hao, walichagua kipotoshi B; *Mawili* wakihusisha mgawanyo wa Sura za Makka na Madinah, jambo ambalo halikuwa sahihi kwani halikufanywa kipindi cha Mtume na wala halikuagizwa na yeye. Wengine walichagua kipotoshi C; *Matatu*, ambalo pia sio sahihi na halina asili yoyote katika migawanyo ya Qur'an. Vilevile, wapo waliochagua kipotoshi D; *Thelathini,* ambacho pia hakikuwa sahihi. Wanafunzi hao, walichanganya idadi ya juzuu zilizopo katika Mus'hafu na mafungu yaliyotajwa na Mtume (S.A.W) katika kuihifadhi, kuiandika na kuikusanya Qur'an.

Kipengele cha (vii) mwanafunzi alitakiwa kubainisha hoja inayoonesha umuhimu wa kushushwa Qur'an kidogo kidogo kwa muda wa miaka 23. Swali hili lilipima uwezo wa mwanafunzi kuelewa historia ya kushuka Qur'an na hekima zake. Wanafunzi mahiri katika mada ya Qur'an, waliweza kujbu kipengele hiki kwa usahihi kwa kuchagua herufi D; *Kutoa nafasi kwa waumini kuihifadhi na kuitekeleza.* Hoja hii imebainishwa wazi katika Qur'an yenyewe na ni ishara ya mapenzi ya Mwenyezi Mungu (S.W) kwa waja wake, kwani kama ingeteremshwa yote kwa mara moja, ingekuwa tabu kwa waumini kuihifadhi na kuitekeleza.

Wanafunzi walioshindwa kujibu kipengele hiki kwa usahihi, walionesha kukosa maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Qur'an. Baadhi yao walichagua vipotoshi A; *Kutoa nafasi ya maandalizi ya kuihifadhi kimaandishi* na B; *Kurahisiha juu ya mchakato wa usomaji na uandishi wake.* Hoja hizo hazikuwa sahihi kwakuwa sio msingi wa kucheleshwa ushukaji wa Qur'an, kwani makusudio ya Qur'an sio sauti za usomwaji wake na uandishi, bali utekelezaji wa maamrisho yake na kujiepusha na makatazo yake. Mambo hayo, yalihitaji muda kwakuwa yalihusisha mabadiliko ya kitabia kwa watu, ambao waliishi katika ujinga kwa muda mrefu sana. Wengine walichagua kipotoshi C; *Kutoa nafasi kwa maswahaba kufanya shughuli zingine*, hili pia halikuwa sahihi kwani maisha ya maswahaba (R.A) hayakuwa na mstari unaotenganisha mambo yao binafsi na Uislamu, muda wote waliishi wakitafuta radhi za Mwenyezi Mungu (S.W) hadi kufariki kwao.

Kipengele cha (viii) mwanafunzi alitakiwa kubainisha vipengele muhimu vinavyotumika katika kuhakiki ukamilifu wa Hadithi. Kipengele hiki kilipima uwezo wa mwanafunzi kuelewa uchambuzi wa Hadithi za Mtume (S.A.W) na uthabiti wake. Aidha, wanafunzi mahiri katika mada ya Sunnah na Hadithi, waliweza kubaini jibu sahihi na kuchagua herufi B; *Isnad, Matini na Rawi,* wanafunzi hao walielewa kuwa hizo ni sehemu tatu za msingi, ambazo Hadithi yoyote inaangaliwa ili kuthibitishwa au kukanushwa.

Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki, baadhi yao walichagua kipotoshi A; *Isnad, Rawi na Mutawatir,* na C; *Isnad, Matini na Mutawatir*, ambavyo havikuwa sahihi kwasababu ndani yake kuna *Mutawatir*, ambayo ni aina ya Hadithi na sio kipengele katika Hadithi. Wengine walichagua kipotoshi na D; *Isnad, Mutawatir na Riwaya,* ambacho pia hakikuwa sahihi kwasababu Riwaya ni aina ya uandishi, maneno au simulizi ya maudhui moja kwa namna tofauti na sio kipengele katika vipengele vikuu vya uhakiki wa Hadithi.

Katika kipengele cha (ix) mwanafunzi alitakiwa kubainisha hoja iliyoibua na kuonesha umuhimu wa Sayansi ya Hadithi. Kipengele hiki kilimpima mwanafunzi uchambuzi wa historia ya uandishi wa Hadithi za Mtume (S.A.W) na matokeo yake katika ulimwengu wa Kiislamu. Wanafunzi mahiri katika historia ya uchambuzi na uhakiki wa Hadithi,

waliweza kubaini jibu sahihi na kuchagua herufi C; *Kutambua Hadithi sahihi na zisizo sahihi.* Wanafunzi hao walionesha kuifahamu vema historia ya Hadithi na hasa njia zilizotumika kuifadhi chanzo hiki muhimu cha sharia.

Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki walionesha kukosa maarifa ya kutosha kuhusu historia ya uandishi wa Hadithi kwa ujumla. Baadhi ya wanafunzi hao walichagua vipotoshi A; *Kutambua vigezo vya uchujaji wa Hadithi,* B; *Kutambua historia ya waandishi wa hadithi*, na wengine walichagua D; *Kutambua historia ya wapokezi wa Hadithi*. Hoja hizo hazikuwa sahihi ingawa katika uchambuzi wa Hadithi husika, vyote hivyo vinaangaliwa. Kwa ujumla vigezo hivyo, ndivyo vinavyopitiwa ili kubaini usahihi wa Hadithi na havikuwa mwisho wa malengo bali malengo makuu yalikuwa ni kutambua Hadithi sahihi na zisizo sahihi.

Kipengele cha (x) mwanafunzi alitakiwa kubaini hoja iliyosababisha ulimwengu kutajwa kuwa katika kipindi cha Jahiliyyah katika karne ya 6 A.D. Kipengele hiki kilipima uwezo wa mwanafunzi kutathmini historia ya wanadamu kabla ya kuja Mtume Muhammad (S.A.W) katika nyanja mbalimbali za maisha. Wanafunzi weledi katika mada ya Bara Arab Zama za Jahiliyah, waliweza kujibu kwa usahihi kwa kuchagua herufi D; *Maovu ya aina mbalimbali yalienea.* Jibu hilo ni muhtasari unaojumuisha mambo mengi maovu na machafu, ambayo yalitamalaki wakati huo. Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na ushirikina, zinaa, kamari, ubabe, mauaji kwa wasio na hatia.

Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki, walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Historia kabla ya kuja kwa Mtume (S.A.W), hivyo majibu yao yalikuwa yakubahatisha. Baadhi yao walichagua kipotoshi A; *Hapakuwa na mafundisho yoyote ya Dini.* Hoja hii haikuwa sahihi kwani yalikuwepo bado mabaki ya mafundisho ya dini kwa jamii ndogo sana kama vile Mayahudi na Manasara (Wakristo), lakini sehemu kubwa hazikuweza kubadilisha hali hiyo. Wengine walichagua kipotoshi B; *Maisha yalikuwa katika zama za mawe.* Hii pia haikuwa hoja sahihi kwani zama za mawe ni zama za kusadikika, historia ya Uislamu inafundisha kuwa mwanadamu hajawahi kupita katika zama za ujima tokea mwanzo wa kuletwa kwake

hapa duniani. Wapo pia waliochagua herufi C; *Watu hawakuwa na chanzo cha maarifa*, jambo ambalo pia sio sahihi kwani chanzo cha maarifa kwa mujibu wa Uislamu ni Allah (S.W), nae anawapa waja wake kwa njia mbalimbali na hajawahi kuacha kufanya hivyo. Kielelezo 1.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali la 1 na kielelezo Na. 1.2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali hilo.

1. Katika kipengele (i) – (x), chagua jibu sahihi kisha **andika herufi yake** katika kisanduku.

(i) Kwa kuzingatia mtazamo wa Uislamu juu ya dhana ya elimu, ni kipengele gani kinabainisha mgawanyo sahihi wa elimu?
A Elimu dunia na elimu akhera
B Elimu ya mwongozo na elimu ya Qur'an
C Elimu ya mazingira na elimu ya shule
D Elimu ya mwongozo na elimu ya mazingira
[D]

(ii) Bainisha hoja inayoeleza kazi kuu ya Dini katika maisha kwa mujibu wa Uislamu.
A Kuweka njia ya mahusiano baina ya watu
B Kuwanusuru watu katika namna zote za uonevu
C Kufafanua asili ya wanadamu na malengo yao
D Kukamilisha hitajio la mtu kiroho na kiitikadi
[B]

(iii) Ukipewa nafasi ya kwenda kuhiji Makka kwa kigezo cha kuzingatia aina ya Hija iliyo nafuu kwa mtu anayetoka mbali, utachagua aina gani?
A *Tamattu* B *Qiran*
C *Umrah* D *Infraad*
[A]

(iv) Ni kafara gani anatekeleza mtu aliyevunja kiapo halali kwa mujibu wa Uislamu?
A Kufunga miezi mitatu bila kuacha
B Kufunga siku saba mfululizo
C Kufunga siku tatu mfululizo
D Kufunga miezi miwili
[C]

(v) Mzee Faki ni baba mwenye mke mmoja ambaye ni mjamzito na wana watoto wanne, mmoja kati yao ni wa kulea ambaye si Muislamu. Ni kiasi gani cha nafaka anapaswa kutoa kwa ajili ya Zakatul-Fitr?
A Kg. 10 B Kg. 12.5
C Kg. 15 D Kg. 17.5
[B]

(vi) Katika mchakato wa kuhifadhiwa Qur'an, hapo mwanzo Mtume (S.A.W) aliwaamrisha maswahaba wake kukusanya na kuiandika Qur'an katika mafungu mangapi?
A Saba B Mawili
C Matatu D Thelathini
[A]

(vii) Hoja gani inabainisha umuhimu wa kushuka Qur'an kidogo kidogo kwa muda wa miaka 23?
A Kutoa nafasi ya maandalizi ya kuihifadhi kimaandishi
B Kurahisisha mchakato wa usomaji na uandishi wake
C Kutoa nafasi kwa Masahaba kufanya shughuli zingine
D Kutoa nafasi kwa waumini kuihifadhi na kuitekeleza
[D]

(viii) Hadithi kamilifu inahakikiwa katika vipengele gani muhimu?
A Isnad, Rawi na Mutawatir
B Isnad, Matin na Rawi
C Isnad, Matin na Mutawatir
D Isnad, Mutawatir na Riwaya
[B]

(ix) Bainisha hoja iliyoibua na kuonesha umuhimu wa sayansi ya Hadithi.
A Kutambua vigezo vya uchujaji wa Hadithi
B Kutambua historia ya waandishi wa Hadithi
C Kutambua Hadithi sahihi na zisizo sahihi
D Kutambua historia ya wapokezi wa Hadithi
[C]

(x) Kwa nini katika karne ya 6 A.D ulimwengu unatajwa kuwa katika kipindi cha Jahiliyyah?
A Hapakuwa na mafundisho yoyote ya dini
B Maisha yalikuwa katika zama za mawe
C Watu hawakuwa na chanzo cha maarifa
D Maovu ya aina mbalimbali yalienea
[D]

**Kielelezo 1.1** Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 1

1. Katika kipengele (i) – (x), chagua jibu sahihi kisha **andika herufi yake** katika kisanduku.

(i) Kwa kuzingatia mtazamo wa Uislamu juu ya dhana ya elimu, ni kipengele gani kinabainisha mgawanyo sahihi wa elimu?
A Elimu dunia na elimu akhera
B Elimu ya mwongozo na elimu ya Qur'an
C Elimu ya mazingira na elimu ya shule
D Elimu ya mwongozo na elimu ya mazingira

[ A ]

(ii) Bainisha hoja inayoeleza kazi kuu ya Dini katika maisha kwa mujibu wa Uislamu.
A Kuweka njia ya mahusiano baina ya watu
B Kuwanusuru watu katika namna zote za uonevu
C Kufafanua asili ya wanadamu na malengo yao
D Kukamilisha hitajio la mtu kiroho na kiitikadi

[ D ]

(iii) Ukipewa nafasi ya kwenda kuhiji Makka kwa kigezo cha kuzingatia aina ya Hija iliyo nafuu kwa mtu anayetoka mbali, utachagua aina gani?
A *Tamattu* B *Qiran*
C *Umrah* D *Infraad*

[ C ]

(iv) Ni kafara gani anatekeleza mtu aliyevunja kiapo halali kwa mujibu wa Uislamu?
A Kufunga miezi mitatu bila kuacha
B Kufunga siku saba mfululizo
C Kufunga siku tatu mfululizo
D Kufunga miezi miwili

[ A ]

(v) Mzee Faki ni baba mwenye mke mmoja ambaye ni mjamzito na wana watoto wanne, mmoja kati yao ni wa kulea ambaye si Muislamu. Ni kiasi gani cha nafaka anapaswa kutoa kwa ajili ya Zakatul-Fitr?
A Kg. 10 B Kg. 12.5
C Kg. 15 D Kg. 17.5

[ A ]

(vi) Katika mchakato wa kuhifadhiwa Qur'an, hapo mwanzo Mtume (S.A.W) aliwaamrisha maswahaba wake kukusanya na kuiandika Qur'an katika mafungu mangapi?
A Saba B Mawili
C Matatu D Thelathini

[ B ]

(vii) Hoja gani inabainisha umuhimu wa kushuka Qur'an kidogo kidogo kwa muda wa miaka 23?
A Kutoa nafasi ya maandalizi ya kuihifadhi kimaandishi
B Kurahisisha mchakato wa usomaji na uandishi wake
C Kutoa nafasi kwa Masahaba kufanya shughuli zingine
D Kutoa nafasi kwa waumini kuihifadhi na kuitekeleza

[ B ]

(viii) Hadithi kamilifu inahakikiwa katika vipengele gani muhimu?
A Isnad, Rawi na Mutawatir
B Isnad, Matin na Rawi
C Isnad, Matin na Mutawatir
D Isnad; Mutawatir na Riwaya

[ C ]

(ix) Bainisha hoja iliyoibua na kuonesha umuhimu wa sayansi ya Hadithi.
A Kutambua vigezo vya uchujaji wa Hadithi
B Kutambua historia ya waandishi wa Hadithi
C Kutambua Hadithi sahihi na zisizo sahihi
D Kutambua historia ya wapokezi wa Hadithi

[ B ]

(x) Kwa nini katika karne ya 6 A.D ulimwengu unatajwa kuwa katika kipindi cha Jahiliyyah?
A Hapakuwa na mafundisho yoyote ya dini
B Maisha yalikuwa katika zama za mawe
C Watu hawakuwa na chanzo cha maarifa
D Maovu ya aina mbalimbali yalienea


[ A ]

**Kielelezo Na. 1.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya swali la 1

### 2.1.2 Swali la 2: Nguzo za Uislamu

Swali hili lilitoka katika mada ya Nguzo za Uislamu katika mada ndogo ya Zakat. Katika swali hili mwanafunzi alitakiwa kuoanisha maelezo ya makundi ya wanaostahiki kupewa Zakat, yaliyokuwa katika orodha A (i) – (v) na majina ya makundi hayo yaliyokuwa katika orodha B (A) - (G), kwa kuandika herufi ya jibu sahihi katika jedwali alilopewa. Swali hili lilipima umahiri wa mwanafunzi kuelewa makundi ya watu wanaostahiki kupewa Zakat kwa mujibu wa Uislamu.

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi wote 104,014 (100%) waliofanya upimaji huu. Kati yao wanafunzi 54,386 (52.29%) walipata alama 2 na 3, ambao ni ufaulu wa wastani na wanafunzi 31,566 (30.35%) walipata alama 4 na 5, ambao ni ufaulu mzuri. Aidha, wanafunzi 18,062 (17.36%) walipata alama 0 na 1, ambao ni ufaulu dhaifu. Muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao ni kama unavyoonekana katika Chati Na. 2.




**Chati Na. 2**: *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 2.*

Chati Na. 2 inaonesha kuwa ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri, ambapo asilimia 82.64 ya wanafunzi waliofanya swali hili, walipata

alama 3 hadi 5, ikilinganishwa na asilimia 17.36 ya wanafunzi waliopata alama za chini (0 na 1).

Wanafunzi waliofanya vizuri katika swali hili, walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya Nguzo za Uislamu hasusan nguzo ya Zakat, ambayo ilipimwa katika swali. Aidha, uchambuzi wa majibu ya wanafunzi hao katika kila kipengele ni kama ifuatavyo:

Kipengele cha (i) mwanafunzi alitakiwa kubaini jina linalotumika kutambulisha kundi la watu wasioweza kumudu mahitaji yao ya kila siku mpaka wasaidiwe. Ambapo, wanafunzi mahiri katika Fiqh ya Zakat, waliweza kujibu kipengele hiki kwa usahihi kwa kuchagua herufi D; *Fukara.* Wanafunzi hao walielewa vema kuwa istilahi hiyo, inapotumika kueleza kundi la wastahiki wa Zakat, inamaanisha watu ambao hawana kipato cha kuendesha maisha yao, hivyo hawawezi kumudu mahitaji yao ya msingi ya kila siku.

Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki, baadhi yao walichagua herufi E; *Masikini* na wengine C; *Watumwa*. Istilahi hizo hazikuwa sahihi kwa sababu hazitoshelezi maelezo yaliyotolewa katika kipengele hicho. Aidha, waliochagua herufi C walishindwa kutofautisha matumizi ya istilahi maskini na fukara, kwakuwa kijamii maneno hayo yanatumika kama kisawe, ilihali ni maneno yenye kueleza tabaka tofauti za watu. Kwa upande mwingine, waliochagua kipotoshi C, walionesha kuchanganya dhana ya utumwa, wakitazama kuwa mtumwa ni mtu asiyemiliki chochote bali yeye ndiye mmilikiwa, hivyo mahitaji yake yote hutimizwa na bwana wake.

Kipengele cha (ii) mwanafunzi alitakiwa kubaini jina la kundi la watu walioharibikiwa njiani, kwa kuibiwa au kuishiwa matumizi yao muhimu. Wanafunzi walioelewa vema maelezo hayo, waliweza kuchagua herufi ya jibu sahihi A; *Ibnu Sabiil*. Wanafunzi hao walielewa kuwa istilahi hiyo, iliyoazimwa katika lugha ya Kiarabu, inaenea makundi yote yaliyotajwa katika maelezo ya kipengele hiki.

Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki, miongoni mwao wapo waliochagua kipotoshi B; *Fi sabilillah* na G; *Al aamilina Alayha.* Machaguo hayo hayakuwa sahihi kwa sababu hayaendani na maelezo yaliomo katika kipengele hiki. Aidha, machaguo

haya yameashiria kuwa wanafunzi hawa hawakuelewa lugha iliyotumika, hivyo walichagua vipotoshi hivyo kwa msingi wa kubahatisha, kwakuwa majina ya makundi hayo yametoholewa katika lugha ya Kiarabu.

Kipengele cha (iii), katika kipengele hiki mwanafunzi alitakiwa kubainisha jina la kundi la wanaostahiki kupewa Zakat, ambao wanafanya shughuli za kuhuisha Dini ya Uislamu. Wanafunzi wenye kufahamu vema makundi ya wastahiki wa Zakat, walijibu kwa usahihi kipengele hiki kwa kuchagua herufi B; *Fisabilillah*. Wanafunzi hao waliielewa vema istilahi hiyo, inayotumika katika Zakat na vile inavyowezesha shughuli mbalimbali zenye kuleta tija na ustawi kwa Dini ya Kiislamu.

Kwa upande mwingine, wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hiki, wengi kati yao walionesha kubahatisha katika majibu yao, kwakuwa hawakujua maana ya istilahi mbalimbali hususan zenye asili ya Kiarabu. Wengine walihusisha maelezo ya kipengele hicho na matokeo ya shughuli za midahalo ya kidini, hivyo walichagua herufi F; *Waliosilimu* wakitumia uzoefu kuwa kundi hilo ndilo maarufu kufanya shughuli za kuhuisha Dini ya Kiislamu.

Katika kipengele cha (iv), mwanafunzi alitakiwa kubaini jina la kundi la wenye kustahiki kupewa Zakat, kwa kuwa wametezwa nguvu au kumilikiwa. Wanafunzi weledi wa Fiqh ya Zakat, waliweza kujibu kipengele hicho kwa usahihi kwa kuchagua herufi C; *Watumwa*. Wanafunzi hao, walionesha kuwa mahiri katika nguzo ya Zakat, wakitambua kuwa mali ya Zakat hutumika pia kwa ajili ya kuwakomboa watumwa.

Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hiki, baadhi yao walichagua kipotoshi E; *Masikini,* kwa dhana kuwa maskini ni tabaka la watu wasio na nguvu hivyo, mara nyingi wanakuwa watumishi wa matajiri, tafsiri ambayo si sahihi. Kadhalika, wengine walichagua kipotoshi D; *Fukara,* kwa muktadha uleule, kwakuwa maneno hayo yanatumika kama visawe katika jamii.

Kipengele cha (v), mwanafunzi alitakiwa kubainisha jina la kundi la watu waliopungukiwa mahitaji muhimu ya kila siku, hivyo kustahiki

kupewa Zakat. Wanafunzi mahiri katika mada ya Zakat, waliweza kubaini kundi hilo kwa usahihi na kuchagua herufi E; *Masikini*. Wanafunzi hao, walielewa vyema dhana ya umasikini kisheria na istilahi, inayotumika kutambulisha kundi hilo kwa mujibu wa Uislamu.

Walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki, wengi walichagua kipotoshi D; *Fukara.* Wanafunzi hao walishindwa kutofautisha tafsiri ya istilahi masikini na fukara, kwakuwa kijamii maneno hayo yanatumika kama visawe, ilihali ni maneno yenye kueleza tabaka mbili tofauti za watu. Wengine walichagua vipotoshi B; *Fisabilillah* na G; *Al aamilina Alayha*. Waliochagua vipotoshi hivi, walionesha kukosa maarifa kuhusu Zakat na kujaribu kubahatisha kutokana na kushindwa kuelewa maana zake. Sampuli ya majibu sahihi na yasiyo sahihi ya wanafunzi katika swali hili yameoneshwa katika kielelezo Na. 2.1 na 2.2. mtawalia.

Oanisha maelezo ya makundi ya wanaostahiki kupewa Zaka katika **Orodha A** na majina ya makundi hayo katika **Orodha B** kisha andika herufi ya jibu sahihi katika sehemu ya kuandikia majibu uliyopewa.

| **Orodha A** | | **Orodha B** | |
|---|---|---|---|
| (i) | Wasioweza kumudu mahitaji yao ya kila siku mpaka wasaidiwe. | A | *Ibnu Sabiil* |
| | | B | *Fi Sabilillah* |
| (ii) | Walioharibikiwa njiani kwa kuibiwa au kuishiwa matumizi yao muhimu. | C | Watumwa |
| | | D | Fukara |
| (iii) | Wanaofanya shughuli za kuhuisha Dini ya Uislamu. | E | Maskini |
| (iv) | Waliotezwa nguvu au kumilikiwa. | F | Waliosilimu |
| (v) | Waliopungukiwa na mahitaji muhimu ya kila siku. | G | *Al Aamilina Alayha* |

**Majibu**

| **Orodha A** | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
|---|---|---|---|---|---|
| **Orodha B** | D | A | B | C | E |

**Kielelezo Na. 2.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 2

Oanisha maelezo ya makundi ya wanaostahiki kupewa Zaka katika **Orodha A** na majina ya makundi hayo katika **Orodha B** kisha andika herufi ya jibu sahihi katika sehemu ya kuandikia majibu uliyopewa.

| **Orodha A** | | **Orodha B** | |
|---|---|---|---|
| (i) | Wasioweza kumudu mahitaji yao ya kila siku mpaka wasaidiwe. | A | *Ibnu Sabiil* |
| | | B | *Fi Sabilillah* |
| (ii) | Walioharibikiwa njiani kwa kuibiwa au kuishiwa matumizi yao muhimu. | C | Watumwa |
| | | D | Fukara |
| (iii) | Wanaofanya shughuli za kuhuisha Dini ya Uislamu. | E | Maskini |
| (iv) | Waliotezwa nguvu au kumilikiwa. | F | Waliosilimu |
| (v) | Waliopungukiwa na mahitaji muhimu ya kila siku. | G | *Al Aamilina Alayha* |

**Majibu**

| **Orodha A** | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
|---|---|---|---|---|---|
| **Orodha B** | E | B | F | D | C |

**Kielelezo Na. 2.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 2


## 2.2 Sehemu B: Majibu Mafupi

Sehemu hii ilikuwa na maswali saba ya majibu mafupi (3, 4, 5, 6, 7, 8 na 9). Mwanafunzi alitakiwa kujibu maswali yote. Maswali hayo yaliandaliwa kutoka katika mada za; *Kumjua Mwenyezi Mungu, Mtazamao wa Uislamu Juu ya Ibada, Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti wa Kiislamu, Qur'an, Sunnah na Hadithi, Historia katika Uislamu* na *Bara Arab Zama za Jahiliyyah karne ya 6 A.D.*

### 2.2.1 Swali la 3: Kumjua Mwenyezi Mungu

Swali hili lilitoka katika mada ndogo ya *Njia za Kumjua Mwenyezi Mungu,* ambapo mwanafunzi alitakiwa kubainisha njia tano, zinazomwezesha mwanadamu kutambua uwepo wa Mola wake katika maisha. Swali lilipima uwezo wa mwanafunzi kuchambua njia hizo, ambazo Mwenyezi Mungu (S.W) amemuwekea mwanadamu, ili aweze kutambua uwepo wake na kumuwezesha kutimiza wajibu wake wa kuumbwa.


Takwimu zinaonesha kuwa kati ya wanafunzi 104,014 (100%) waliofanya swali hili, wanafunzi 55,523 (53.38%) walipata alama 2.5 hadi 6, ambao ni ufaulu wa wastani. Wanafunzi wengine 31,800 (30.57%) walipata alama 0 hadi 2, ambao ni ufaulu dhaifu. Na wanafunzi 16,691 (16.05%) walipata alama 6.5 hadi 10, ambao ni ufaulu mzuri. Muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao kwa asilimia ni kama unavyoonekana katika Chati Na. 3.




**Chati Na. 3**: *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 3*

Chati Na. 3 inaonesha kuwa ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa asilimia 69.43 ya wanafunzi, walifaulu kwa kupata alama kuanzia 2.5 hadi 10, ikilinganishwa na asilimia 30.57 ya wanafunzi waliopata alama za chini.

Uchambuzi uliofanywa katika majibu ya wanafunzi, umeonesha kuwa waliofaulu katika swali hili, walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya Kumjua Mwenyezi Mungu (S.W) na walielewa vema matakwa ya swali. Wanafunzi hao, waliweza kubainisha njia zinazomwezesha mwanadamu kutambua uwepo wa Mola wake katika maisha, kama zilivyobainishwa katika Qur'an na Sunnah. Hoja ambazo wanafunzi hao walizitoa ni kama vile; (i) *Fitra,* (ii) *Nafsi ya mwanadamu,* (iii) *Vipaji vya mwanadamu,* (iv) *Mazingira yanayomzunguka mwanadamu,* na (v) *Wahyi*. Kielelezo Na. 3.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyefaulu katika swali hili.



3. Bainisha njia tano zinazomwezesha mwanadamu kutambua uwepo wa Mola wake katika maisha.

(i) Nafasi ya fitra (maumbile)
Kila mwanadamu amepandikizwa hisia za kimaumbile zitakazo muwezesha kumtambua mola wake kwa usahihi

(ii) Vipaji vya mwanadamu
Vipaji vya mwanadamu kama vile milango ya fahamu akili na vipawa vingine alivyotunukiwa ni ishara tosha ya uwepo wa Allah: au nyenzo pekee ikitumiwa vizuri huweza kumtambua Allah (s.w)

(iii) Nafsi ya mwanadamu
Nafsi ya mwanadamu kama vile msukumo wa damu mwilini, mmeng'enyo wa chakula ni ishara tosha ya kuwepo kwa Allah (s.w)

(iv) Mazingira
Utegemezi wa maliasili katika mazingira ya wanadamu, wanyama, mimea ni ishara ya uwepo wa Allah:

(v) Wahyi
Ni kitekemba kutoka kwa Allah (s.w) kwenda kwa mitume na kuwafundisha wanadamu fani zote za elimu alizoteremshiwa na Allah (s.w).

**Kielelezo Na. 3.1** Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 3


Uchambuzi zaidi uliofanywa katika majibu ya wanafunzi, ulibaini kuwa waliopata ufaulu wa chini katika swali hili, baadhi yao walikosa maarifa kuhusu njia za kumjua Mwenyezi Mungu (S.W). Miongoni mwao, walitoa hoja zilizotokana na juhudi zao binafsi kwa namna walivyofikiria. Wanafunzi hao walitoa hoja kama vile: *Kuwepo kwa madhehebu mbalimbali, Kuwepo kwa vitu vya ajabu vinavyomzunguka bimadamu, MwenyeziMungu anatenda maajabu,* pamoja na *Upaji wa pekee*. Hoja hizi ziliashiria kuwa wanafunzi hao hawakuwa na maarifa kuhusu mada ya kumjua Mwenyezi Mungu (S.W), hivyo walifanya jitihada binafsi za kufikiria.

Mwanafunzi mmoja aliandika: *Kufanya ibada na kumtaka msamaha Mola wako, Kufunga Sunnah na hata mwezi mtukufu wa Ramadhan, Kufanya ihsan kwa watu unaowajua na usio wajua, uswali swala za usiku na Kumuomba Mwenyezimungu akufungulie mlango wa Imani na Kutoa Zakat na Sadaka.* Hoja hizi hazikuwa majibu ya swali bali, mwanafunzi alitaja baadhi ya matendo ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu kiibada, sio njia za kutambua uwepo wake.

Wanafunzi wengine walishindwa kuelewa matakwa ya swali, na kujibu kinyume na yaliyoulizwa. Miongoni mwao, wapo waliotaja njia za mawasiliano kati ya Mwenyezi Mungu (S.W) na waja wake, badala ya

njia zinazomwezesha mwanadamu kutambua uwepo wa Mola wake. Mmoja kati ya wanafunzi hao aliandika; *Ilham, Nyuma ya pazia, Ndoto za kweli* na *Kutumwa malaika*. Majibu haya yalionesha kuwa wanafunzi huyu alikuwa na maarifa kuhusu mada ya Kumjua Mwenyezi Mungu, isipokuwa alishindwa kuzingatia matakwa ya swali. Hivyo, hoja alizotoa mwanafunzi huyo hazikujibu swali la msingi aliloulizwa.

Kadhalika, wengine walichanganya kati ya njia zinazo muwezesha mwanadamu kutambua uwepo wa Mola wake na Nguzo za Imani, ambapo mmoja kati ya wanafunzi hao aliandika: *Kuamini Malaika, Kuwepo kwa Siku ya mwisho, Kuamini vitabu, na Kuamini Mitume wa Mwenyezimungu*. Hoja hizi, zilibainisha nguzo za imani ya Kiislamu, sio njia za kumtambua Mwenyezi Mungu (S.W). Kielelezo Na. 3.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi, aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.



3. Bainisha njia tano zinazomwezesha mwanadamu kutambua uwepo wa Mola wake katika maisha.

(i) kutamka shahada

(ii) kusimamisha swala tano

(iii) kutoa zakat

(iv) kufunga Mwezi mtukufu wa kwa Ramadhani

(v) kwenda kuhiji Makka kwa mtu Mwenye uwezo


**Kielelezo Na. 3.2** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 3.

Katika kielelezo Na. 3.2 mwanafunzi ameorodhesha nguzo za Uislamu, badala ya njia zinazomwezesha kutambua uwepo wa Mola wake. Majibu hayo, yanaonesha mwanafunzi alishindwa kuelewa msingi wa swali husika.

### 2.2.2 Swali la 4: Mtazamo wa Uislamu Juu ya Ibada

Swali lilikuwa na vipengele vitatu (a), (b) na (c), kutoka katika mada ya Mtazamo wa Uislamu Juu ya Ibada. Swali lilipima umahiri wa wanafunzi kuchambua dhana ya ibada kwa Muislamu na athari zake katika maisha ya kila siku. Katika kipengele cha 4 (a), mwanafunzi alitakiwa kufafanua dhana ya ibada kisheria, kwa kuakisi maelekezo ya jumla ya Mwenyezi Mungu (S.W) katika Qur'an (51: 56): *''Sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu''*. Aidha, katika kipengele cha 4 (b), mwanafunzi alitakiwa kubainisha mahusiano yaliyopo kati ya *Ibada maalumu* na maisha ya Muislamu ya kila siku. Vilevile, katika kipengele 4 (c), mwanafunzi alitakiwa kubainisha sababu ya kuwepo kwa maumbile yote, yaliyomzunguka mwanadamu.

Takwimu zinaonesha kuwa wanafunzi wote 104,014 (100%), walifanya swali hili. Kati yao 60,346 (58.02%), walipata alama 0 hadi 2.5, ambao ni ufaulu dhaifu. Wanafunzi 38,233 (36.76%), walipata alama za 3 hadi 6, ambao ni ufaulu wa wastani. Aidha, wanafunzi 5,435 (5.23%), walipata alama 6.5 hadi 10, ambao ni ufaulu mzuri. Chati Na. 4. inaonesha muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao kwa asilimia.




**Chati Na. 4**: *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 4*

Chati Na. 4. inaonesha kuwa ufaulu wa wanafunzi katika swali hili, ulikuwa wa wastani kwani asilimia 36.76 ya wanafunzi, walipata alama 2.5 hadi 10, ikilinganishwa na asilimia 58.02 ya wanafunzi, waliopata ufaulu wa chini.

Uchambuzi uliofanyika katika majibu ya wanafunzi, umeonesha kuwa wanafunzi waliofaulu katika swali hili, walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya ibada kwa mujibu wa Uislamu, walielewa vema matakwa ya swali. Kwa sababu hizo, waliweza kutumia maarifa yao vizuri katika kujibu swali hilo kwa usahihi. Kwa mfano, katika kipengele 4 (a), walieleza dhana ya ibada kisheria kuwa: *Kumtumikia Allah (S.W) kikamilifu kwa kufuatta maarisho na kuacha makatazo yake yote*. Kielelezo Na. 4.1 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi la mwanafunzi.

4. "Sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu" Qur'an (51:56). Kwa mujibu wa aya hiyo;
(a) Fafanua dhana ya ibada kisheria.

ni kumtumikia mwenyezimungu kwa kufuata maamrisho na ku acha makatazo yake yote hapa ulimwenguni

**Kielelezo Na. 4.1** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 4(a)


Katika kujibu kipengele cha 4 (b), wanafunzi hao waliweza kubainisha mahusiano yaliyopo kati ya ibada maalumu na maisha ya Muislamu ya kila siku kwa kueleza kuwa; *Ibada maalumu ni kama vile Swala, Funga, Zakat, Hijja nk, ndio nyenzo kuu za kumuandaa na kumwezesha muumini kumuabudu na kumtumikia Allah(SW), katika kila kipengele cha maisha ya binafsi, kifamilia, na kijamii*. Kielelezo Na. 4.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyefaulu.

(b) Bainisha mahusiano yaliyopo kati ya *Ibada maalumu* na maisha ya Muislamu ya kila siku.

ibada maalumu humuwezesha muislamu kumtambua na kumuabudu mola wake mfano wa ibada maalumu ni kama vile Hijjah, swala, ibada n.k katika maisha ya kila siku

**Kielelezo Na. 4.2** Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 4(b)

Aidha, katika kujibu kipengele cha 4 (c), wanafunzi waliofanya vizuri, waliweza kubainisha sababu ya kuwepo maumbile yaliyomzunguka mwanadamu kwa kuandika; *Lengo lake kuu ni kumtumikia mwanadamu ili kufikia lengo la kuumbwa kwake kwa kuboresha maisha yake. Pia maumbile na viumbe vyote vinavyomzunguka mwanadamu, vimetiishwa kwake ili aweze kuvitumia katika kutekeleza ibada*, Qur'an (4;13). Kielelezo Na. 4.3 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi aliyefaulu.


(c) Bainisha sababu ya kuwepo kwa maumbile yote yaliyomzunguka mwanadamu.
Ni kwa sababu ya kumuwezesha mwanadamu kuweza kufikia lengo la kuumbwa kwake hapa ulimwenguni

**Kielelezo Na. 4.3** Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 4 (c)

Uchambuzi zaidi uliofanywa katika majibu ya wanafunzi, unaonesha kuwa waliopata ufaulu hafifu katika swali hili, baadhi yao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Mtazamo wa Uislamu juu ya Ibada, huku wengine wakishindwa kubaini matakwa ya swali.

Katika kipengele cha 4 (a), ambacho mwanafunzi alitakiwa kufafanua dhana ya ibada kisheria kwa muktadha wa aya aliyopewa, mmoja kati ya wanafunzi hao, aliandika kuwa; *Mwanadamu ameumbwa kwa ajili ya kumuabudu Allah, sikuwaumba majini na watu ili wapate kuniabudu*. Maelezo haya yaliashiria kuwa mwanafunzi alikosa maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya ibada katika Uislamu, hivyo badala ya kufafanua dhana ya ibada, alinukuu lengo la kuumbwa kama lilivyotajwa katika aya iliyotangulia. Mwingine alieleza kuwa; *Ibada ni kinga na bila ibada hakutakuwa na utii wala dini,* Maelezo haya yalionesha faida za ibada na sio maana ya ibada. Mwingine aliandika; *Dhana ya ibada ni kitendo cha kuamini Mwenyezimungu yupo lakini hauna nia*, maelezo haya yanaonesha kukosa maarifa kuhusu dhana ya ibada kwa ujumla, hivyo mwanafunzi alitoa majibu ya kubuni ambayo pia yalikuwa yanapishana.

Mwingine, alieleza umuhimu wa ibada katika Uislamu, badala ya kufafanua dhana ya ibada, ambapo alieleza kuwa; *Ibada ni lazima kwa mwanadamu kwa sababu pindi mwanadamu anapofanya ibada anajiweka karibu yeye na Mola wake*. Kielelezo Na. 4.4 kinaonesha

sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi

4. "Sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu" Qur'an (51:56). Kwa mujibu wa aya hiyo;

(a) Fafanua dhana ya ibada kisheria.

dhana ya Ibada ni kitendo cha kuamini mwenyezi mungu yuko lakini hauna n'a.

**Kielelezo Na. 4.4** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi swali la 4 (a)

Katika kielelezo Na. 4.4 mwanafunzi alionesha kukosa maarifa kuhusu dhana ya ibada kisheria, hivyo alitoa majibu ya kubuni ambayo pia yalikuwa yanapishana.

Katika kipengele cha 4 (b), ambacho wanafunzi walitakiwa kuonesha mahusiano baina ya ibada maalumu na maisha ya Muislamu, wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi, baadhi yao walishindwa kuifasiri istilahi hiyo kwa ujumla wake, na kuieleza kama aina ya Sala. Mfano, mmoja kati ya wanafunzi hao aliandika; *Ibada maalumu huswaliwa na mtu yeye mwenyewe kwa kuomba kitu kwa mola wake mlezi na maisha ya muislamu ya kila siku ni kuswali kama kawaida na waislamu wengine kama ilivyozoeleka*.

Mwingine aliandkia; *Ibada maalumu ni ibada inayoswaliwa kila wakati swala tano na maisha ya muislamu ya kila siku ni kufuata maamrisho ya Allah*. Kadhalika mwingine, akaeleza kuwa; *Ibada maalumu ni aina ya ibada ambayo huswali kwa ajili ya kumcha Mungu na maisha ya kila siku ambayo tunaishi kwa ajili ya kumcha Allah (SW)*. Majibu ya wanafunzi hawa, yalionesha kuwa walikosa maarifa kuhusu maana ya ibada maalumu na hata malengo yake pia. Kielelezo Na. 4.5 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi katika kipengele 4 (b).

(b) Bainisha mahusiano yaliyopo kati ya *Ibada maalumu* na maisha ya Muislamu ya kila siku.

Ni kitendo cha kumuomba mungu MAISHA YA MUISLAMU. Ni kitendo cha kuwa duniani kutembea na kutazama vitu Ulivuhuru mungu.

**Kielelezo Na. 4.5** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 4 (b)

Katika kielelezo Na. 4.5 mwanafunzi alishindwa kubainisha mahusiano kati ya ibada maalumu na maisha ya Muislamu, badala yake alitoa maelezo yaliyoashiria kueleza kitendo badala ya uhusiano.

Katika kipengele cha 4 (c), ambacho wanafunzi walitakiwa kubainisha sababu ya kuwepo kwa maumbile yaliyomzunguka mwanadamu, wanafunzi walioshindwa kujibu kipengele hiki kwa usahihi, walitoa hoja mbalimbali, ambazo ni kinyume na matakwa ya swali. Kuna aliyehusisha maumbile hayo na nguzo ya kwanza ya Uislamu na Imani. Nae alieleza; *Kuamini kuwa yupo Mwenyezimungu mmoja tu, kwa sababu hapana Mola apaswa kuabudiwa kwa haki isipokuwa yeye Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na mwenye kurehemu*. Mwingine alibainisha asili ya maumbile hayo badala ya sababu ya kuwepo. Mwanafunzi huyo alieleza; *Sababu ya kuwepo kwa maumbile yote hapa duniani ni Allah (SW)*, *Sababu ya kuwepo maumbile yote ni Mwenyezimungu pekee yake ndiye amesababisha*.

Mwingine alichanganya maumbile yanayo mzunguka mwanadamu na viungo vya mwili wa mwanadamu. Wanafunzi hawa wali toa hoja kama; *kwa sababu kila umbile lina kazi yake kama mdomo kutaja jina la Allah, Kusoma Qur'an, Kuimba qaswida* na *kutamkisha shahada*. Mwingine alisema; *kwa sababu ili watu waweze kuoana na kuijaza dunia.* Majibu haya hayakuwa sahihi na kuashiria kuwa wanafunzi hawakulielewa swali la msingi. Kielelezo Na. 4.6 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi katika kipengele 4 (c).

(c) Bainisha sababu ya kuwepo kwa maumbile yote yaliyomzunguka mwanadamu.

Kwa sababu kila umbile lina kazi yake kama mdomo kutaja jina la allah, Kusoma Qur'an, kuimba Qaswida, na Kutamkisha shahada.


**Kielelezo Na. 4.6** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 4 (c)

Katika kielelezo Na. 4.6 mwanafunzi ameeleza kazi za viungo mbalimbali vya mwanadamu badala ya kubainisha sababu za maumbile yaliyomzunguka.

### 2.2.3 Swali la 5: Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti wa Kiislamu

Swali hili lilitoka katika mada ya *Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti wa Kiislamu*. Swali lilikuwa na vipengele viwili 5 (a) na 5 (b), ambapo katika kipengele 5 (a) mwanafunzi alitakiwa kubainisha mambo sita muhimu anayopaswa kufanyiwa mtu anayekaribia kufariki, wakati 5 (b) mwanafunzi alitakiwa kuainisha mambo manne ya faradhi anayostahiki kufanyiwa maiti wa Kiislamu. Swali hili lilipima umahiri wa wanafunzi kutumia maarifa ya mada hii katika kumuandaa maiti wa Kiislamu.


Swali lilijibiwa na wanafunzi wote 104,014 (100%) waliofanya upimaji huu. Kati yao wanafunzi 73,920 (71.07%) walipata alama 6.5 hadi 10, ambao ni ufaulu mzuri. Wanafunzi 27,932 (26.85%) walipata alama 2.5 hadi 6, ambao ni ufaulu wa wastani na wanafunzi 2,162 (2.08%) walipata alama 0 hadi 2, ambao ni ufaulu dhaifu. Muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao ni kama unavyoonekana katika Chati Na. 5.




**Chati Na. 5:** *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 5*

Chati Na. 5. inaonesha kuwa ufaulu wa wanafunzi katika swali hili, ulikuwa mzuri kwani asilimia 97.92 ya wanafunzi walipata alama 2.5 hadi 10, ambazo ni alama za kufaulu, ikilinganishwa na asilimia 2.08 ya wanafunzi waliopata alama 0 hadi 2.5.

Uchambuzi uliofanyika katika majibu ya wanafunzi, unaonesha waliofaulu vizuri katika swali, walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada iliyoulizwa na walielewa vema matakwa ya swali. Katika kipengele cha 5 (a), wanafunzi hao walieleza mambo mbalimbali anayopaswa kufanyiwa mtu anayekaribia kufariki kama vile; (i) *Kumpigisha mswaki, (ii) Kumuogesha, (iii) Kumtia manukato, (iv) Kumlaza kwa ubavu wa kulia na kumuelekeza Qibla, (v) Kumpa maji ya kunywa, (vi) Kutamka kalima ya Laa ilaaha ilallah bila ya kumuashiria yeye kutamka, nk.* Kielelezo Na. 5.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika kipengele hicho.


5. (a) Bainisha mambo sita muhimu anayopaswa kufanyiwa mtu anayekaribia kufariki.

(i) Kumpa maji, mtu anaekaribia kufa anapaswa kupewa maji ili asife akafa akiwa na njaa au kiu

(ii) Kumlaza ubavu wa kuume (kulia), mtu anaekaribia kufa anapaswa kulazwa ubavu wa kulia, akielekea qibla.

(iii) Kumtamkia shahada, kumtamkia kalima tukufu ya laila haila llah Muhammadu rasulu llwah

(iv) Kumuogesha, mtu anaekaribia kufa anapaswa kuogeshwa na kuwa safi muda wote.

(v) Kumpigisha mswaki, mtu anaekaribia kufa inabidi apigishwe mswaki ili kinywa chake kiwe safi muda wote

(vi) Kumtilisha udhu, mtu anaekaribia kufa inabidi atilishwe udhu, ili aweze kuwa twahara muda wote na hata kuelekezw

**Kielelezo Na. 5.1:** Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 5 (a)

Aidha, katika kipengele cha 5 (b) wanafunzi hao waliweza kuainisha mambo manne ya faradhi anayostahiki kufanyiwa maiti wa Kiislamu, kama yalivyobainishwa na sharia. Wanafunzi hao waliyataja mambo hayo kwa ufasaha kuwa ni; (i) *Kumuosha, (ii) Kumkafini (kumvisha sanda), (iii) Kumsalia na (iv) Kumzika*. Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika kipengele hicho.

(b) Ainisha mambo manne ya Faradhi anayostahiki kufanyiwa maiti wa Kiislamu

(i) Maiti ya kiislamu hupaswa kuoshwa

(ii) Maiti ya kiislamu hupaswa kuvikwa sanda

(iii) Maiti ya kiislamu hupaswa kuswaliwa

(iv) Maiti ya kiislamu hupaswa kuzikwa

**Kielelezo Na. 5.2:** Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 5 (b).

Ama, kwa upande wa wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi swali hili, baadhi yao hawakuelewa matakwa ya swali na wengine hawakuwa na maarifa, kuhusu mada ya Mambo ya lazima kufanyiwa Maiti wa Kiislamu.

Miongoni mwa wanafunzi ambao hawakuelewa vema matakwa ya swali katika kipengele cha 5 (a), mmoja wao alitaja; *Kumfunika maiti kwa shuka kubwa nyeupe, kumswalia, kumfumbisha macho maiti, kumfunga mdomo kwa kitambaa* na *kumlainisha viungo*. Majibu haya hayakuwa sahihi kwa kuwa mambo hayo anafanyiwa Muislamu mara tu baada ya kufariki.

Wengine walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada hii, ambapo miongoni mwao aliandika; *kumlaza chali na kifudifudi, kuveshwa nguo, kutoa wosia, ndugu zake wanapaswa watoe nafaka kwa ajili ya zakatul fitr, na anapaswa kutii na kunukuu maneno ya mtu yule anayekwenda kufariki*. Majibu haya yaliashiria kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada, hivyo walijibu kwa kubahatisha. Kielelezo Na. 5.3 Kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi katika kipengele cha 5 (a).

5. (a) Bainisha mambo sita muhimu anayopaswa kufanyiwa mtu anayekaribia kufariki.

(i) Kuswali sana

(ii) Kuomba msamaha

(iii) Kufunga ramadhan nasunah

(iv) Kusoma Qur'an

(v) Kusikilidha mawaidha na hadith

(vi) kuhadheka na kama anapeleka kwendakuhiji makka

**Kielelezo Na. 5.3:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 5(a).

Katika kipengele cha 5 (b), ambacho mwanafunzi alitakiwa kuainisha mambo manne ya faradhi anayostahiki kufanyiwa maiti wa Kiislamu. Baadhi ya wanafunzi, walishindwa kubaini matakwa ya swali, na wengine walikosa maarifa kuhusu mada iliyoulizwa. Wanafunzi hao waliandika mambo mbalimbali ambayo si sahihi. Miongoni mwao aliandika; *Kumswalia mtume (S.A.W), Kusoma audhubillah kabla ya suratul fatiha, Kusema aamin baada ya kusoma Suratul fatiha, Kutoa takbira ya kwanza, Kuswali karibu na kichwa cha maiti na Kwa ndugu jamaa na marafiki kumuombea dua*. Majibu haya yalitaja baadhi ya vipengele vya kutekeleza Sala ya maiti, badala ya mambo ya lazima anayostahiki kufanyiwa maiti. Mwingine alieleza; *Kwa kumlipia madeni yake kama alimkopesha, Kwa kuchangisha mali zake na Kuwapelekea yatima*. Hoja hizi pia hazikuwa sahihi kwa sababu mwanafunzi alieleza haki zinazohusu mali za mtu aliyefariki. Kielelezo Na. 5.4 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.

(b) Ainisha mambo manne ya Faradhi anayostahiki kufanyiwa maiti wa Kiislamu.

(i) Nia

(ii) takbira ya kuhirimia

(iii) Kumsomea Suratul fatha

(iv) Mtume muhammad (s.a.w) kama alivyo faradhwis


**Kielelezo Na. 5.4:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 5 (b).

Katika kielelezo Na. 5.4, mwanafunzi ameshindwa kutaja mambo ya faradhi anayopaswa kufanyiwa maiti wa Kiislamu, badala yake ametaja baadhi ya nguzo za Sala ya maiti.

### 2.2.4 Swali la 6: Qur'an

Swali hili lilitoka katika mada ya Qur'an mada ndogo ya Kushuka na kuhifadhiwa Qur'an. Katika swali hili, mwanafunzi alitakiwa kupanga historia ya kushuka Qur'an kwa Mtume (S.A.W), katika mtiririko sahihi kwa kuandika namba 1-5, chini ya namba ya kirumi katika jedwali alilopewa. Swali hili lilipima uwezo wa mwanafunzi kuchambua matukio muhimu katika kushuka na kuhifadhiwa kwa Qur'an, kama ambavyo Qur'an yenyewe na Hadithi za Mtume (S.A.W) zimebainisha.

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi wote 104,014 (100 %) waliofanya upimaji huu. Kati yao wanafunzi 71,183 (68.44 %) walipata alama 0 hadi 2, ambao ni ufaulu dhaifu. Wanafunzi 28,842 (27.73%) walipata alama 2.5 hadi 6, ambao ni ufaulu wa wastani na wanafunzi 3,989 (3.84%) walipata alama 6.5 hadi 10, ambao ni ufaulu mzuri. Muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao ni kama unavyoonekana katika Chati Na. 6.




**Chati Na. 6:** *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 6*

Chati Na. 6. inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani asilimia 31.56 ya wanafunzi hao walipata alama 2.5 hadi 10, ikilinganishwa na asilimia 68.44 ya wanafunzi waliopata alama za chini (0 hadi 2).

Uchambuzi uliofanyika katika majibu ya wanafunzi, ulionesha kuwa ufaulu wa wastani katika swali hili ulisababishwa na ukosefu wa maarifa ya kutosha katika historia ya kushuka kwa Qur'an, hivyo wanafunzi wengi walipata baadhi ya vipengele na kukosa vingine. Aidha, walikuwepo wanafunzi mahiri waliofaulu kwa ukamilifu, ambapo waliweza kupanga matukio hayo kwa usahihi, kama yalivyohifadhiwa na historia. Mtiririko sahihi wa matukio hayo ulikuwa; *3-Kabla ya Qur'an Mtume (S.A.W) alikuwa akipata Wahyi kwa ndoto, 5-Qur'an yote kwa ujumla ilihifadhiwa katika ubao mtukufu wa Allah (S.W) katika Arshi yake, 1-Kutoka humo ikamfikia Mtume (S.A.W) kwa hatua kupitia Malaika Jibril (A.S) kwa miaka 23. 2-Mwanzo wa kushuka kwake alipokea Mtume (S.A.W) aya tano za mwanzo za Suratul Alaq*. Kielelezo Na. 6.1 Kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali hili.

6. Panga historia ya kushuka Qur'an kwa Mtume (S.A.W) katika mtiririko sahihi kwa kuandika namba 1- 5 katika sehemu ya kuandikia majibu uliyopewa.
   (i) Kutoka humo ikamfikia Mtume (S.A.W) kwa hatua kupitia Malaika Jibril (A.S) kwa miaka 23.
   (ii) Mwanzo wa kushuka kwake alipokea Mtume (S.A.W) Aya tano za *Surat Alaq*.
   (iii) Kabla ya Qur'an Mtume (S.A.W) alikuwa akipata wahyi kwa ndoto.
   (iv) Qur'an ilishushwa kutoka *Lawhi mahfudh* mpaka mbingu ya kwanza.
   (v) Qur'an yote kwa ujumla ilihifadhiwa katika ubao mtukufu wa Allah (S.W) katika Arshi yake.

**Majibu**

| (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
|---|---|---|---|---|
| 3 | 5 | 4 | 1 | 2 |


**Kielelezo Na. 6.1:** Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 6.

Katika kielelezo Na. 6.1 mwanafunzi aliweza kupangilia matukio ya historia ya kuteremka Qur'an kwa usahihi, kama yalivyotajwa katika historia.

Uchambuzi zaidi uliofanywa katika majibu ya wanafunzi, umeonesha kuwa wanafunzi waliopata ufaulu hafifu katika swali hili, hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu historia ya kushuka na kuhifadhiwa Qur'an. Wengi kati ya hao walibuni mpangilio wao, ambao ulikuwa ukipishana

katika matukio. Mmoja kati ya wanafunzi hao aliandika; *4 - Qur'an ilishushwa kutoka Lauhilmahfudh mpaka mbingu ya kwanza, 5 - Qur'an yote kwa ujumla ilihifadhiwa katika ubao mtukufu wa Allah (S.W) katika Arshi yake, 2- Mwanzo wa kushuka kwake alipokea mtume (S.A.W) aya tano za mwanzo za suratul Alaq, 3-Kabla ya Qur'an Mtume (S.A.W) alikuwa akipata wahyi kwa ndoto, 1-Kutoka humo ikamfikia Mtume (S.A.W) kwa hatua kupitia Malaika Jibril (A.S) kwa miaka 23*. Mpangilio huu haukuwa sahihi na ulionesha kuwa wanafunzi hao walishindwa kuelewa vema historia ya kushuka Qur'an.

Mwingine alipanga kwa mtiririko; *5 - Qur'an yote kwa ujumla ilihifadhiwa katika ubao mtukufu wa Allah (S.W) katika Arshi yake, 4 - Qur'an ilishushwa kutoka Lauhilmahfudh mpaka mbingu ya kwanza, 2, Mwanzo wa kushuka kwake alipokea Mtume (S.A.W) aya tano za mwanzo za suratul Alaq, 3 - Kabla ya Qur'an Mtume (S.A.W) alikuwa akipata Wahyi kwa ndoto, 1- Kutoka humo ikamfikia Mtume (S.A.W) kwa hatua kupitia Malaika Jibril (A.S) kwa miaka 23*. Mtiririko huu pia hauko sawa kwa kuwa unapishana na historia halisi ya kushuka Qur'an. Kielelezo Na. 6.2 Kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi katika swali la 6.



6. Panga historia ya kushuka Qur'an kwa Mtume (S.A.W) katika mtiririko sahihi kwa kuandika namba 1- 5 katika sehemu ya kuandikia majibu uliyopewa.
   (i) Kutoka humo ikamfikia Mtume (S.A.W) kwa hatua kupitia Malaika Jibril (A.S) kwa miaka 23.
   (ii) Mwanzo wa kushuka kwake alipokea Mtume (S.A.W) Aya tano za *Surat Alaq*.
   (iii) Kabla ya Qur'an Mtume (S.A.W) alikuwa akipata wahyi kwa ndoto.
   (iv) Qur'an ilishushwa kutoka *Lawhi mahfudh* mpaka mbingu ya kwanza.
   (v) Qur'an yote kwa ujumla ilihifadhiwa katika ubao mtukufu wa Allah (S.W) katika Arshi yake.

**Majibu**

| (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
|---|---|---|---|---|
| ~~iii~~ v | iii | ii | iv | i |


**Kielelezo Na. 6.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya swali la 6

Katika kielelezo Na. 6.2, mwanafunzi alishindwa kupangilia matukio ya historia ya kuteremka Qur'an kwa usahihi, kwa kuwa alikosa maarifa ya kutosha kuhusu mada hii.

### 2.2.5 Swali la 7: Sunnah na Hadithi

Swali hili lilitoka katika mada ya *Sunnah na Hadithi*, katika mada ndogo ya *Uchambuzi wa Hadithi za Mtume* (S.A.W). Katika swali hili mwanafunzi alitakiwa kubainisha vigezo vitano vinavyotumika kutambua hadithi isiyo sahihi kwa kuzingatia matini. Swali lilipima uwezo wa mwanafunzi kuchambua vigezo vya matini katika utambuzi wa Hadithi.

Takwimu zinaonesha kuwa kati ya wanafunzi 104,014 (100%) waliofanya upimaji huu, wanafunzi 88,854 (85.43%) walipata alama 0 hadi 2, ambao ni ufaulu hafifu. Wanafunzi 9,677 (9.30%) walipata alama 2.5 hadi 6, ambao ni ufaulu wa wastani na wanafunzi 5,483 (5..27%) walipata alama 6.5 hadi 10, ambao ni ufaulu mzuri. Aidha, kati ya wanafunzi waliokuwa na ufaulu hafifu, wanafunzi 78,989 (75.90%) walipata alama 0. Chati Na. 7 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao kwa asilimia.




**Chati Na. 7:** *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 7*

Chati Na. 7. inaonesha kuwa, ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa dhaifu kwani asilimia 85.43 ya wanafunzi walipata alama 0 hadi 2, ikilinganishwa na asilimia 14.57 ya wanafunzi waliofaulu.

Uchambuzi unaonesha kuwa ufaulu wa chini katika swali hilo, ulisababishwa na wanafunzi kukosa maarifa kuhusu mada ya Sunnah na Hadithi na wengine kushindwa kubaini matakwa ya swali husika. Baadhi ya wanafunzi walioelewa vibaya swali hilo, waliandika vigezo vya matini, vinavyothibitisha usahihi wa Hadithi, badala ya vigezo vinavyokanusha. Wanafunzi hao waliandika; *Matini isimzushie Mtume jambo lolote, matini isiahidi adhabu kali kwa kosa dogo na malipo makubwa kwa amali ndogo, Hadithi isipingane na Qur'an, Hadithi isipingane na uhalisia, Hadithi izingatie kuwa matini yake isikatike*. Hoja hizo hazikuwa sahihi kwa kuwa zilieleza chanya badala ya hasi. Hali hiyo inaashiria kuwa wanafunzi hao hawakuelewa vema matakwa ya swali.

Wengine walichanganya na vipengele mbalimbali vinavyotumika katika uchambuzi wa Hadithi. Kuna walioanisha Hadithi kwa kigezo cha usahihi. Wanafunzi hao waliandika; *Hadthi sahihi, Hasan, Dhaifu, na Maudhuu'*. Kundi lingine la wanafunzi hao walieleza Hadithi kwa kigezo cha umashuhuri, ambapo waliandika; *Hadithi Mutawatir na Ahad*. Kadhalika, wapo waliotaja vigezo vya ukamilifu wa Hadithi ambavyo ni *Isnad, Matini na Rawi*. Majibu hayo hayakuwa sahihi kwa mujibu wa matakwa ya swali.

Wanafunzi ambao walishindwa kujibu kwa usahihi kwa sababu ya kukosa maarifa walitoa hoja mbalimbabali za kubuni ambazo hazikuwa sahihi. Mmoja kati ya hao aliandika; *Matamshi ya maneno, Awe na elimu ya dini ya Kiislamu, Kuandika kwa kutumia lugha ya mkato, Kufuata mwongozo na sheria za uandishi, Iwe na hadithi za mitume na Malaika wake na awe na elimu ya dini ya Kiislamu*.

Mwingine aliandika; *Kuwa na historia tofauti tofauti ya Mtume (S.A.W), Kuwa na ushindani wa uandishi wa vitabu, Kuwa na vitabu visivyo na hadithi ya Mtume (S.A.W).* Mwingine alikuja na hoja kama vile; *Wahusika wake, Kuandika historia ya Mtume, Ubora wa hadithi hiyo, Chanzo, wakati na mahali hadithi hiyo iliandikwa, Hadithi isiyokuwa na wahusika na hadithi kutokuwa na mwanzo wa kueleweka*. Majibu hayo yote hayakuwa mantiki kwa muktadha wa swali, zaidi yaliashiria kuwa wanafunzi hao hawakuwa maarifa kabisa kuhusu mada ya Sunnah na

Hadithi. Kielelezo Na. 7.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi katika swali la 7.

7. **Bainisha vigezo vitano vinavyotumika kutambua Hadithi isiyo sahihi kwa kuzingatia matini.**

(i) Hadithi isiwe inapingana na qur'an

(ii) Hadithi isiwe inaahidi mapato makubwa kwa tendo dogo na mateso makubwa kwa kosa dogo.

(iii) Isiwe inapingana na ukweli wa kihistoria (historical fact)


(iv) Isiwe inapingana na ukweli ambao hauwezi kubadilika

(v) Isiwe inamzushie mambo ya uongo mtume muhammadi (S.AW)

**Kielelezo Na. 7.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 7

Katika kielelezo Na. 7.1 mwanafunzi ameandika vigezo vya matini vinavyothibitisha Hadithi sahihi na sio Hadithi isiyo sahihi. Mwanafunzi anaonesha ameshindwa kutambua matakwa ya swali husika.

Uchambuzi zaidi uliofanywa katika majibu ya wanafunzi, unaonesha kuwa wanafunzi waliofaulu katika swali hili, walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu sayansi ya Hadithi na walielewa vema matakwa ya swali. Aidha, wanafunzi hao waliweza kubainisha vigezo hivyo vinavyotumika kutambua Hadithi isiyo sahihi kwa kuzingatia matini na kuviandika kwa ufasaha. Miongoni mwa vigezo walivyoeleza ni pamoja na; *Hadithi kuwa na maneno ya uongo ndani yake, Kupingana na Qur'an, Ikimzulia uongo Mtume (SAW), Ikipingana na Hadithi nyingine iliyo thibitika kuwa ni sahihi, Ikiahidi adhabu kali kwa kosa dogo sana, Ikiahidi malipo makubwa sana kwa wema mdogo* na *Ikipingana na uhalisia*. Kielelezo Na. 7.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu kwa usahihi katika swali hili.



7. Bainisha vigezo vitano vinavyotumika kutambua Hadithi isiyo sahihi kwa kuzingatia matini.

(i) kama hadithi inapingana na aya za Qur-an

(ii) kama hadithi inapingana na hadithi nyingine zilizo thibitishwa kuwa ni sahihi

(iii) kama hadithi ina mzulia mtume (s.a.w) kwa mutendo aliyoyafanya kulingania dini wakati wa utume wake.

(iv) kama hadithi hiyo ina sema uongo na wapokezi wake wanakinzana


(v) kama hadithi hiyo ina ahidi adhabu kubwa kwa uovu ndogo na malipo au thawabu nyingi kwa amali ndogo

**Kielelezo Na. 7.2:** sampuli ya majibu sahihi katika swali la 7

### 2.2.6 Swali la 8: Historia katika Uislamu.

Swali lilikuwa na vipengele vitatu (a), (b) na (c), kutoka katika mada ya *Historia katika Uislamu*, mada ndogo ya *Dhana juu ya historia*. Katika swali hili mwanafunzi alipimwa umahiri wake katika kuchambua masuala ya msingi, yanayojenga mwelekeo wa mwanadamu katika maisha yake binafsi na mahusiano yake na wengine. Aidha, mwanafunzi alitakiwa kufafanua katika kipengele cha 8 (a); Asili ya mwanadamu, 8 (b); Lengo la mwanadamu na 8 (c); Hadhi na wajibu wa mwanadamu.


Takwimu zinaonesha kuwa wanafunzi wote 104,014 (100%) waliofanya upimaji huu walifanya swali hili. Kati yao wanafunzi 59,449 (57.15%) walipata alama 2.5 hadi 6, ambao ni ufaulu wa wastani. Wanafunzi 29,887 (28.73%) walipata alama 0 hadi 2, ambao ni ufaulu dhaifu, na wanafunzi 14,678 (14.11%) walipata alama 6.5 hadi 10, ambao ni ufaulu mzuri. Chati Na. 8. inaonesha muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao kwa asilimia.




**Chati Na. 8**. *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 8*

Chati Na. 8 inaonesha kuwa ufaulu katika swali hili, ulikuwa mzuri kwani asilimia 71.27 ya wanafunzi walipata kati ya alama 2.5 hadi 10, ikilinganishwa na asilimia 28.73 ya wanafunzi waliopata alama za chini (0 hadi 2).

Wanafunzi waliofaulu katika swali hili, walionesha kuwa mahiri katika mada ya Historia katika Uislamu na walielewa vema matakwa ya kila kipengele cha swali hili. Aidha, katika kipengele cha 8 (a), ambacho mwanafunzi alitakiwa kueleza asili ya mwanadamu kwa mujibu wa Uislamu, wanafunzi hao walifafanua kwa usahihi na ufaha kuwa; *Kwa mujibu wa Uislamu ni mwanadamu ni kiumbe aliyeumbwa katika umbile halisi la kiutu hivyo hatokani na mabadiliko yoyote ya kimaumbile. Tokea kuumbwa kwake alipewa vipawa mbalimbali kama vile ufahamu na akili ili aweze kuendana na mazingira aliyowekewa. Au mwanadamu ameumbwa na Allah (S.W) kutokana na udongo na roho*. Kielelezo Na. 8.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyefaulu katika kipengele cha 8(a).



8. Utambuzi binafsi na mwelekeo wa mwanadamu unategemea tafsiri aliyonayo juu ya mambo matatu ya kihistoria. Fafanua mambo hayo kwa mujibu wa Uislamu.

(a) Asili ya mwanadamu

Asili ya mwanadamu ni Udongo, Mwanadamu ameumbwa kwa udongo.

**Kielelezo Na. 8.1:** Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 8(a)

Kadhalika, katika kipengele cha 8 (b), ambacho mwanafunzi alitakiwa kufafanua lengo la maisha ya mwanadamu, wanafunzi mahiri katika historia waliweza kufafanua kuwa; *Lengo kuu la kuumbwa mwanadamu na kuletwa hapa duniani ni kumtumikia (kumuabudu) Mwenyezimungu (S.W) pekee, hivyo shughuli zote anazofanya mwanadamu ni visaidizi vya kumfikisha katika hatua hiyo*. Kielelezo Na. 8.2 Kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali hili.


(b) Lengo la mwanadamu

lengo la kuletwa mwanadamu ni: kuweza kumuabudu Mwenyezimungu katika kila kipengele cha maisha yake: kama ibada, kijamii, kisiasa na kiuchumi.

**Kielelezo Na. 8.2:** Sampuli ya majibu sahihi ya kipengele cha 8(b).

Vilevile, katika kipengele cha 8 (c), ambacho mwanafunzi alitakiwa kufafanua hadhi na wajibu wa mwanadamu, wanafunzi hao waliweza kufafanua kuwa; *Mwenyezimungu (S.W) amempa mwanadamu hadhi ya kuwa khalifah au kiongozi mwenye wajibu wa kusimamia sharia za Mwenyezimungu hapa duniani na kuhakikisha uadilifu kwa viumbe vyote.* Kielelezo Na. 8.3 Kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali 8 (c).

(c) Hadhi na wajibu wa mwanadamu

kwa Mujibu wa Uislamu hadhi ya mwanadamu ni kuwa khalifa na wajibu ni kumuabudu allah na kufanya yale aliyoamrisha na kuacha yale aliyokataza.

**Kielelezo Na. 8.3:** Sampuli ya majibu sahihi ya kipengele cha 8 (c)

Uchambuzi zaidi uliofanyika katika majibu ya wanafunzi, umeonesha kuwa wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika swali hili, waligawanyika katika makundi mawili. Kundi la kwanza walishindwa kubaini matakwa ya swali na la pili walionesha kukosa maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Historia katika Uislamu, hivyo walishindwa kujibu ipasavyo.

Katika kipengele cha 8 (a), ambacho mwanafunzi alitakiwa kufafanua kuhusu asili ya mwanadamu, wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi, walitoa maelezo yaliyotofautiana baina yao. Mmoja kati ya wanafunzi hao alieleza; *Ni maumbile ya mwanadamu na vipaji, Aliumbwa kwa asili yake mwenyewe*. Mwingine aliandika*; Ni ile hali ya mwanadamu kuwa na hali fulani, Kwanza amjue muumba wake*. Na mwingine aliandika; *Asili ya mwanadamu ni kuswali, kuomba kwa Mola ili akushushie wahyi.* Si hayo tu, mwanafunzi mwingine alieleza asili ya mwanadamu kuwa; *Ni mambo au vitu anavyofanya mwanadamu kulingana na tabia alizonazo*. Majibu hayo yote, yalionesha wazi kuwa wanafunzi hao walikosa maarifa kuhusu dhana ya historia kwa mujibu wa Uislamu. Kielelezo Na. 8.4 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hicho.


8. Utambuzi binafsi na mwelekeo wa mwanadamu unategemea tafsiri aliyonayo juu ya mambo matatu ya kihistoria. Fafanua mambo hayo kwa mujibu wa Uislamu.

(a) Asili ya mwanadamu

~~ya~~ Asili ya mwanda waku tofauti asli yu kike na asli ya kiume.

**Kielelezo Na. 8.4 :** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya kipengele cha 8 (a)

Kipengele 8 (b), ambacho mwanafunzi alitakiwa kufafanua lengo la maisha ya mwanadamu, baadhi ya wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi, walileta ufafanuzi uliotofautiana baina yao vilevile. Miongoni mwao kuna aliyeandika kuwa lengo la mwanadamu; *Ni mambo au ndoto aliyonayo mwanadamu kwa ajili ya maisha yake ya kila siku*, *lengo la mwanadamu ni kufahamu kuwa muumba wake yupo na lengo lake*. Mwingine alifafanua kuwa; *Ni ile hali ya mwanadamu kuwa na lengo katika kitu chochote cha kwake kwenye moyo unalolifikiri*. Majibu haya, yaliashiria kuwa wanafunzi hao hawakuwa na maarifa kuhusu dhana ya lengo la kuumbwa mwanadamu kwa mujibu wa Uislamu. Kielelezo Na. 8.5 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki.



(b) Lengo la mwanadamu

Ni kuja kutimiza amri ya allah (s.w) ili wamuabudu mitu
me

**Kielelezo Na. 8.5:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya kipengele cha 8 (b)

Katika kielelezo Na. 8.5 mwanafunzi ametaja lengo la mwanadamu kuwa ni kutimiza amri ya Allah (S.W) ili wamuabudu Mtume, jambo ambalo ni kinyume kabisa na itikadi ya Uislamu.

Kipengele cha 8 (c), ambacho mwanafunzi alitakiwa kufafanua hadhi na wajibu wa mwanadamu, miongoni mwa wanafunzi ambao hawakujibu kwa usahihi alifafanua kuwa; *Ni ile hali ya mwanadamu kuwa na hadhi na wajibu wa lazima kufanya kitu chochote hicho*, mwingine akaandika; *Ni tabia ya mwanadamu inayomwezesha kufanya jambo au mambo mbalimbali*. Mwingine alijibu kuwa; *Hadhi ni kuwa na fikra na wajibu ni kuswali*. Na mwingine akaleta hoja kuwa; *Ni kuwa yule mtu aliye elimika na kuwa na uelewa wa kielimu ndio wajibu wa mwanadamu amjue Mwenyezimungu mwenye kurehemu na rehema*. Mwingine hakuenda mbali na aliyetangulia, yeye akaeleza kwa ufupi kuwa; *Ni kutii maamrisho ya Allah (S.W) kusaidia wasiojiweza*. Majibu hayo sio

sahihi kwa mujibu wa kipengele hiki, aidha maelezo waliyoyatoa yalionesha kwamba wanafunzi hao walikosa maarifa kuhusu mada ya Historia katika Uislamu. Kielelezo Na. 8.6 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki.

(c) Hadhi na wajibu wa mwanadamu

Hadhi na wajibu wa mwanadamu
Hadhi na wajibu wa mwanadamu ni kuwa yule
yule mtu aliezlimika na kuwa navelewa wakie
Ilimu ndio wajibu wa mwanadamu na anyuwe
mwenyezi mungu wenda kulehemu nawenye lehema


**Kielelezo Na. 8.6:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya kipengele cha 8 (c)

Katika kielelezo Na. 8.6 mwanafunzi amebainisha nyenzo aliyopewa mwanadamu kufikia hadhi na kutimiza wajibu wake lakini hajaeleza hadhi wala wajibu huo.

### 2.2.7 Swali la 9: Bara Arab Zama za Jahiliyyah Karne ya 6 A.D

Swali lilitolewa katika mada ya *Bara Arab Zama za Jahiliyyah* katika mada ndogo ya *Kulingania Uislamu Makkah*. Katika swali hili mwanafunzi alitakiwa kutaja vipengele vitano, vinavyoonesha kuandaliwa kwa Mtume (S.A.W) ki-ilham. Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi kutathmini matukio muhimu katika maisha ya Mtume (S.A.W) kabla ya kupewa utume, ambayo yalionesha kuongozwa kwake na kuhifadhiwa kitabia na mwenendo wake kwa ujumla.

Takwimu zinaonesha kuwa wanafunzi wote 104,014 (100%) waliofanya upimaji huu walijibu swali hili. Kati yao, wanafunzi 68,837 (66.18%) walipata alama 0 hadi 2, ambao ni ufaulu dhaifu. Wanafunzi 21,382 (20.56%) walipata alama 2.5 hadi 6, ambao ni ufaulu wa wastani na wanafunzi 13,795 (13.26%) walipata alama 6.5 hadi 10, ambao ni ufaulu mzuri. Chati Na. 9 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao kwa asilimia.





**Chati Na. 9:** *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 9.*

Chati Na. 9 inaonesha kuwa swali lilikuwa na ufaulu wa wastani, kwani asilimia ya wanafunzi waliofaulu ilikuwa 33.82. Wanafunzi hao walipata alama 2.5 hadi 10, ikilinganishwa na asilimia 66.18 waliopata alama za chini (0 hadi 2).

Wanafunzi waliofaulu katika swali hili walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ndogo ya *Kulingania Uislamu Makkah*, na walielewa vema matakwa ya swali. Wanafunzi hao waliweza kutaja miongoni mwa vipengele vilivyoonesha kuandaliwa kwa Mtume (S.A.W) ki-ilham, kwa hoja mbalimbali kama vile; (i*) Kuhifadhiwa kwa Mtume (S.A.W) tangu akiwa mdogo akaweza kujiepusha kufanya mambo maovu na machafu, jambo hili lilifanya kazi yake ya daawa iwe nyepesi, kwani watu hawakupata historia mbaya kutoka kwake. (ii) Mtume (S.A.W) kumuoa Bi Khadija ambaye alimsaidia katika kazi yake ya daawa kwa kumpa ushauri , maliwazo na msaada mambo ambayo yalimpa nguvu Mtume (S.A.W) kuendelea na kazi yake, kwani alipata nguvu za kiuchumi kupitia mkewe Bi Khadija ambaye alikuwa tajiri pia mke mwema ambaye utajiri wake ulitumika katika kazi ya daawa mwanzo mwa Utume wake. (iii) Mtume (S.A.W) kabla hajapewa utume,*

*alikuwa na tabia njema zilizokuwa za kipekee, hivyo ilikuwa rahisi kuwavutia watu katika Uislamu pale alipoanza kulingania Kutokana na tabia njema za Mtume (S.A.W) alizokuwa nazo kabla ya kupewa utume zilipelekea watu waweze kumuamini pale alipoanza kutangaza kuwa yeye ni Mtume wa Allah kwani hawajawahi kumsikia akisema uongo tangu utotoni mwake. (iv) Kupewa jina la Muhammad na babu yake lenye maana ya mshukuriwa kama ilivyotabiriwa katika vitabu vilivyotangulia. (v) Malezi bora aliyopata kupitia mama yake Bi Halima, babu yake na Ami yake. (vi) Kuchukia maovu na kujitenga pangoni. Tangu akiwa kijana hakupenda kuona maovu na hatimaye alijitenga na kukaa pangoni ili kutekeleza ibada zake.* Kielelezo Na 9.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali la 9.



9. Taja vipengele vitano vinavyoonesha kuandaliwa kwa Mtume Muhammad (S.A.W) kiil-ham.

(i) Tabia yake njema isiyokuwa na mfano kuanzia utoto wake hadi ukubwa wake.

(ii) Kupewa jina la muhamad na babu yake

(iii) Ndoa yake mtume (S.A.W) na bi khadija

(iv) Kuzaliwa katika kabila tukufu la kikureish

(v) malezi bora aliyoyapata kutoka kwa babu yake pamoja na mama yake.


**Kielelezo Na. 9.1:** Sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali la 9

Uchambuzi zaidi uliofanyika katika majibu ya wanafunzi, ulibaini kuwa waliopata alama za chini katika swali hili, walikosa maarifa ya kutosha kuhusu Historia ya Mtume (S.A.W) kabla ya Utume akiwa Makkah na wengine walishindwa kuelewa matakwa ya swali. Mmoja kati ya wanafunzi hao aliandika kazi alizozifanya Mtume (S.A.W) kama vile; *Kuja kusambaza dini ya Allah (S.W), Kuja kuwaokoa watu na majaribu ya shetani, Kuleta ujumbe wa Allah, Kuja kukataza uovu*. Mwingine aliandika; *Kugaiwa ukhalifa wa kuwa Mtume ulimwenguni, Kumuoa Bi Mariam, Kusoma kalima ya kushuhudia kuwa Mungu yupo na anapaswa kupewa sifa zote*. Mwanafunzi huyo alitoa hoja za kubuni ambazo zote hazikuwa sahihi. Mwingine alitaja baadhi ya matukio ya kweli ambayo Mtume alifanyiwa lakini hayakuhusu maandalizi ya ki-

ilham, mwanafunzi huyo alitaja; *Kupasuliwa moyo na kuoshwa kuondoa chuki, kisasi na roho mbaya, Kupewa mafunzo juu ya uislamu na vipengele vyake, Kuelekezwa kuhusu matendo ya kiislamu yaliyo tajwa, Ijtihaad, ilhaam, Qur'an na Ijmaa na Kupewa utume*. Kwa ujumla wanafunzi hao walionesha kukosa maarifa juu ya maandalizi ya Mtume (S.A.W) ki-ilham, hivyo waliandika hoja zao kwa msingi wa kubahatisha.

Baadhi ya wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi, walionesha kushindwa kuelewa matakwa ya swali hilo, hivyo walichanganya matukio mbalimbali ya kihistoria. Mmoja kati ya wanafunzi hao aliandika; *Safari ya Israa na Miraj ambapo aliongea na kupewa mafundisho ili aufikishie ummah wake, Kuonana na Malaika Jibril na kuongozwa katika safari hiyo, Kuswalisha katika Msikiti wa Makkah wakati wakipita kuelekea kwa Allah, Kuongea na Mwenyezi na kisha kukabidhiwa Utume na kushushiwa Qur'an, Kuiona pepo na moto ili aje awape mafunzo watu wake*.

Wengine waliandika njia za mawasiliano baina ya wanadamu na Mwenyezi Mungu (S.W) kama vile; *Ilhaam, kuongea na Mwenyuezimungu nyuma ya pazia, mbao zilizoandikwa, kutumwa malaika na kufikisha kama ilivyo takiwa*. Majibu hayo yalionesha kuwa, wanfunzi ho hawakuelewa matakwa ya swali, kwani matukio aliyoyataja yalihusu safari ya Israa na Miraj na wengine walitaja njia za mawasilano. Kielelezo Na. 9.2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi katika swali hili.


9. Taja vipengele vitano vinavyoonesha kuandaliwa kwa Mtume Muhammad (S.A.W) kiil-ham.

(i) Mtume Muhammad (S.A.W) alikuja ili kuendeleza dini ya Kiislamu

(ii) Mtume Muhammad (S.A.W) Alikuja kuwaelimisha juu ya kuwepo kwa dini ya kiislamu

(iii) Kuja kuwafundisha waumini wake

(iv) Kuja kuwafundisha mema na ~~maovu~~ kuwafundisha yale ambayo ameagizwa na mwenyezimungu (S.A.W)

(v) Mtume Muhammad (S.A.W) Alikuja kuwaelimisha juu ya kuwepo kwa allah (S.A.W) ili wamuabudu

**Kielelezo Na. 9.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya swali la 9

Katika kielelezo Na. 9.2 mwanafunzi alieleza baadhi ya kazi alizozifanya Mtume (S.A.W), badala ya matukio yanayoonesha kuandaliwa kwake ki-ilham.


## 2.3 Sehemu C: Insha

Sehemu hii ilikuwa na swali moja la insha kutoka katika mada ya Nguzo za Uislamu. Swali hilo lilikuwa na alama 15.

### 2.3.1 Swali la 10: Nguzo za Uislamu

Swali lilitoka katika mada ya *Nguzo za Uislamu*, katika mada ndogo ya *Funga*, ambapo mwanafunzi alitakiwa kueleza mambo matano yanayobatilisha ibada ya funga.


Swali lilijibiwa na wanafunzi wote 104,014 (100%) waliofanya upimaji huu. Kati yao wanafunzi 40,607 (39.13%) walipata alama 9.5 hadi 15, ambao ni ufaulu mzuri. Wanafunzi 32,565 (31.31%) walipata alama 0 hadi 4, ambao ni ufaulu dhaifu na wanafunzi 30,752 (29.57%) walipata alama 4.5 hadi 9.0, ambao ni ufaulu wa wastani. Muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao ni kama unavyoonekana katika Chati Na. 10.




**Chati Na. 10:** *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 10*

Chati Na. 10 inaonesha kuwa ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri, kwani asilimia 68.69 ya wanafunzi walipata alama 4.5 hadi 15, ikilinganishwa na asilimia 31.31 ya waliopata alama za chini (0 hadi 4).

Uchambuzi uliofanywa katika majibu ya wanafunzi, umeonesha kuwa kiwango kizuri cha ufaulu kilichofikiwa katika swali hili, ni kwa sababu ya maarifa waliyokuwa nayo wanafunzi kuhusu Nguzo ya Funga na kuelewa vema matakwa ya swali hilo. Miongoni mwa mambo yanayobatilisha ibada ya Funga waliyoyaeleza pamoja na; *Kula na kunywa kwa kusudia, Kujitapisha kwa makusudi, kupatwa na hedhi na nifasi, Kujitoa manii kwa makusudii, Kunuia kula na hali umefunga* na *Kufanya tendo la ndoa mchana wa Ramadhan.* Kielelezo Na 10.1 Kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali hili.



10. Eleza mambo matano yanayobatilisha ibada ya funga (Siyam).

Funga ni nguzo ya nne ya uislamu ambayo inalengo la kumfanya mja kuwa mcha mungu katika dini ya kiislam. Kuna mambo ambayo mtu akifanya mchana wa ramadhani hubatilisha funga yake. Yafuatayo ni mambo yanayobatilisha ibada ya funga;

Kula au kunywa kwa makusudi mchana wa ramadhani, Mtu anapofanya kitendo cha kunywa kitu chochote au kula kitu chochote mchana wa ramadhani husababisha funga yake kuharibika na hatokuwa na uwezo wa kuendelea na funga.

Kujitoa manii kwa makusudi mchana wa ramadhani, Mtu anapoamua kujitoa manii kwa makusudi mchana wa ramadhani husababisha funga yake kubatilika na kushindwa kuweza kuendelea kufanya ibada ya funga tena.

Kufanya jimai mchana wa ramadhani, Mke na mume au mtu yoyote yule ambaye amefunga na anafanya Jimai mchana wa ramadhani basi huyo funga yake itakuwa imebatilishwa na hawezi tena kufunga:

Mwanamke akipokuwa na nifasi au hedhi. Mwanamke ambaye anadamu za hedhi au nifasi yeye hatakuwa kufunga ramadhani mpaka amalize damu za hedhi na ajitwaharishe na aendelee na ibada yake ya funga.

Kunuia kula au kunywa mchana wa ramadhani, Mtu anaponuia nia ya kutaka kula au kunywa mchana wa ramadhani husababisha funga yake kubatilika na kushindwa kuendelea na swaumu yake.

Kwa ujumla, hizi ni vitu baadhi ambavyo vinamsababisha mtu ambaye yupo kwenye funga akivifanya au kuwa navyo vinabatilisha funga yake na hatoweza kuendelea na funga.

**Kielelezo Na 10.1:** Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 10

Uchambuzi zaidi uliofanywa katika majibu ya wanafunzi, ulionesha kuwa walioshindwa kujibu swali hili kwa usahihi walikosa maarifa ya

kutosha kuhusu mada ya Funga, na wengine walishindwa kubaini matakwa ya swali. Baadhi yao walishindwa kueleza hoja walizozitoa ingawa walielewa swali.

Miongoni mwa wanafunzi ambao walionesha kutokuwa na maarifa kuhusu Funga, walitoa hoja kama vile: *Kukosea kanuni na utaratibu, makosa ya ibada, Kusimamisha Uislamu, Kutokwa na mkojo, Kusimamisha swala muda mwingi, Kutokwa na udhu*, *Kufuturisha wenzio na kufanya ibada sana wakati wa usiku*. Mwingine alitoa hoja kuwa; *Kuamka na janaba, Kulala muda mrefu, Kusahau kama umefunga, Kuoga wakati wa mchana na kupiga mswaki mchana, kutoa damu, na kukumbatiana mke na mme*. Hoja hizo hazikuwa sahihi kwa mujibu wa swali, kwani mambo aliyoyataja mwanafunzi ni yale yanayodhaniwa kuwa yanaharibu Funga. Katika mrengo huohuo, yupo alioandika dharura ambazo mtu akiwanazo anaruhusiwa kutofunga, ambazo ni; *Kuwa na maradhi, kuwa katika ujauzito, kutokuwa na tohara, Kuwa katika safari*. Mwingine alieleza sharti za kutosihi kwa Sala, kama vile; *kutokuwa na udhu, kutokuwa na sitara na kuvunjika udhu katika swala.*

Mwanafunzi mwingine aliandika; *Kutoa zakat, swaumu na kuhiji Makka*. Huyu hakuelewa kabisa matakwa ya swali, kwani alitaja baadhi ya nguzo za Uislamu badala ya mambo yayobatilisha Funga. Wapo pia walioandika mambo yanayopunguza thamani ya funga kama; *Kutukana, kusengenya, kumpiga mke wake, kumpiga mtu au kuiba bila ya mwenyewe kuridhia*. Mwingine akaandika; *Kuwinda ukiwa katika vazi la Ihraam*. Hoja hii haikuwa sahihi kwakuwa ilieleza masharti ya Ihraam, ambayo hayahusiani na vibatilishi vya Funga. Majibu haya yanaashiria kuwa wanafunzi hawa, hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu vibatilishi vya funga. Kwa ujumla, majibu hayo yote, hayakuwa sahihi kwa kuwa hayakujibu swali la msingi. Kielelezo namba 10.2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 10.

**10. Eleza mambo matano yanayobatilisha ibada ya funga (Siyam).**

Ibada ya funga ni kitendo cha kufunga na kumpwekesha Allah S.W. taja mambo matano yanayobatilisha ibada ya funga.

Shahada mbili ni kitendo ya kutoa shahada mbili ili mwenye kubatilisha ibada ya funga kama kutoa shahada mbili zinazotoa na shahada mbili zilizowekwa kutumia zinayo batilisha.

Kuhiji kwa mtu aliye na uwezo. Ni kitendo cha kuhiji kwa mtu aliye na uwezo kuenda kuhiji ni kitendo cha kuhiji kwa mtu aliye usiache familia yake ina fedha za wala hivyo watawezakwenda yeyote.

Kusimamisha swala. Ni kitendo cha mtu kusimamisha na hata kama akiwa amini anaweza kusimami swa swala ni mtu na hata hivyo ni kitendo cha kusimisha swala na hata hivyo mtu kwenda kuhiji makkah au kusimisha swala na hata hivyo safarini unaweza kusimamisha swala.

Kuamini Qadari zake unaweza kufunga kwa kumuamini mwenyezi mungu na Qadari zake ku hiji makkah kwa mtu aliye na uwezo Qadari zake za mwenyezi mungu kuamini kadari zake na unamuamini kuamini Qadari zake.

Kuamini ya siku ya mwisho mwenyezi mungu aliseme tuamini siku ya mwisho na hata hiyo siku ya mwisho ipo kwenye nguzo za imani.

Hii ni nguzo ya imani ambayo nguzo za imani kuamini siku ya mwisho inayobatilisha funga ibada kitu muhimu sana na hata hiyo mwisho inayobatilisha nguzo za imani.

Yote kwa yote yanayobatilisha ibada ya funga za imani ya mwanadamu ni mtu aliyeamini sana na hata hivyo mwanadamu ni mtu aliyeamini na hata hivyo ni mwisho wake yanayobatilisha ibada ya funga imani kuamini mwenyezi mungu na ibada zake ibada ni kila kitu ambacho ya mwanadamu ni mtu aliyeamini na hata hiyo imani yake.

**Kielelezo Na. 10.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 10.

Katika kielelezo Na. 10.2 mwanafunzi ameeleza baadhi ya nguzo za Uislamu na Imani badala ya mambo yanayobatilisha ibada ya Funga.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KWA KILA MADA

Katika upimaji huu mada zifuatazo zilihusika; *Mtazamo wa Uislamu Juu ya Dini, Mtazamo wa Uislamu juu ya Elimu, Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti wa Kiislamu (97.92 %) Nguzo za Uislamu (75.67%) Historia Katika Uislamu (71.27%), Kumjua Mwenyezi Mungu (69.43%), Mtazamo wa Uislamu juu ya Ibada (41.98%), Bara Arab zama za Jahiliyyah (33.82%) Qur'an (31.56%)* na mwisho *Sunnah na Hadithi (14.57%)*.

Uchambuzi wa takwimu za matokeo ya wanafunzi kwa mada, umeonesha kuwa kiwango kizuri cha ufaulu kilifikiwa katika mada za *Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti wa Kiislamu (97.92 %) Nguzo za Uislamu (75.67%) Historia Katika Uislamu (71.27%), Kumjua Mwenyezi Mungu (69.43%)*. Vilevile, kulikuwa na ufaulu wa wastani katika mada za *Mtazamo wa Uislamu juu ya Ibada (41.98%), Bara Arab zama za Jahiliyyah (33.82%)* na *Qur'an (31.56%)*. Aidha, mada moja pekee ndio ilikuwa na ufaulu dhaifu, nayo ni *Sunnah na Hadithi (14.57%)* iliyopimwa katika swali la 7.

Ufaulu mzuri katika mada za *Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti wa Kiislamu (97.92 %) Nguzo za Uislamu (75.67%) Historia Katika Uislamu (71.27%)* na *Kumjua Mwenyezi Mungu (69.43%)*, ulichangiwa na maarifa mazuri waliokuwa nayo wanafunzi katika mada hizo, umahiri wa; katika kubaini matakwa ya maswali na uwezo mzuri wa kuwasilisha majibu stahiki kwa ufasaha.

Ufaulu wa wastani katika mada za *Mtazamo wa Uislamu Juu ya Ibada (41.98%), Bara Arab zama za Jahiliyyah (33.82%)* na *Qur'an (31.56%),* ulisababishwa na hali ya wanafunzi kujibu maswali kwa kutoa baadhi ya hoja sahihi na kushindwa hoja zingine. Hali hiyo, iliashiria kuwa wanafunzi hao hawakuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika.

Aidha, ufaulu dhaifu katika mada ya *Sunnah na Hadithi (14.57%),* ulisababishwa na kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika na kushindwa kubaini matakwa ya swali. Takwimu za ufaulu wa kila mada, zimeoneshwa kwenye kiambatisho, ambapo rangi nyekundu inaashiria kiwango cha chini cha ufaulu, rangi ya njano kiwango cha

wastani cha ufaulu na rangi ya kijani inaonesha kiwango kizuri cha ufaulu.

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla, kiwango cha ufaulu katika upimaji huu wa kidato cha pili (FTNA 2024) katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu, kilikuwa kizuri kwa asilimia 71.41. Uchambuzi huu umeonesha changamoto mbalimbali, ambazo hazina budi kutatuliwa ili kuboresha zaidi kiwango hicho katika upimaji unaofuata. Changamoto zilizojitokeza kwa wanafunzi katika kujibu maswali, ni pamoja na kushindwa kubaini matakwa ya maswali na kukosa maarifa ua kutosha katika mada, hususani mada ya *Sunnah na Hadithi (14.57%).*

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha ufaulu katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu yafuatayo yanapendekezwa:

(a) Walimu wawaongoze wanafunzi kujadili katika vikundi na kurejea muhtasari wa somo na vitabu vya kiada na ziada, ili kupata maarifa ya kutosha hususan katika mada ya *Sunnah na Hadithi.*

(b) Walimu waboreshe upimaji endelevu kwa wanafunzi kwa kuwapa maswali yanayopima ngazi za juu za umahiri, ili kukuza uwezo wao kimaarifa.

(c) Wanafunzi wazingatie mbinu za kusoma kwa kuelewa, ili wawe na uwezo wa kubaini matakwa ya swali na hoja sahihi za kujibia.

(d) Walimu watumie taarifa hii ya uchambuzi wa matokeo ya upimaji wa kitaifa, ili kuboresha ufundishaji na kuepuka makosa yanayojitokeza katika kujibu maswali ya somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu.

## Kiambatisho cha Pekee

### Uchambuzi wa Ufaulu wa Wanafunzi katika Mada

| Na. | Mada | Ufaulu wa Kila Swali | | Asilimia ya Wanafunzi waliopata wastani wa alama 30 au zaidi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Namba ya Swali | Asilimia ya Ufaulu | | |
| 1. | Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti Muislamu | 5 | 97.92 | 97.92 | Vizuri |
| 2. | Nguzo za Uislamu | 2 | 82.64 | 75.67 | Vizuri |
| | | 10 | 68.69 | | |
| 3. | Mtazamo wa Uislamu Juu ya Elimu, Mtazamo wa Uislamu Juu ya Dini,Mtazamo wa Uislamu Juu ya Ibada, Nguzo za Uislamu, Qur'an, Sunnah na Hadithi na Bara Arab Zama za Jahiliyyah karne ya 6 A.D | 1 | 74.69 | 74.69 | Vizuri |
| 4. | Historia Katika Uislamu | 8 | 71.27 | 71.27 | Vizuri |
| 5. | Kumjua Mwenyezi Mungu | 3 | 69.43 | 69.43 | Vizuri |
| 6. | Mtazamo wa Uislamu Juu ya Ibada | 4 | 41.98 | 41.98 | Wastani |
| 7. | Bara Arab zama za Jahiliyyah | 9 | 33.82 | 33.82 | Wastani |
| 8. | Qur'an | 6 | 31.56 | 31.56 | Wastani |
| 9. | Sunnah na Hadithi | 7 | 14.57 | 14.57 | Dhaifu |
| **Wastani wa Jumla wa Ufaulu Kwa Mada** | | | | **56.77** | **Wastani** |